Gazeti la kwanza la Islam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Enyi mlioamini, si halali kwenu kuwarithi wanawake kwa nguvu; wala msiwazuie (kuolewa) ili mpate kuwanyang'anya baadhi ya vile mlivyowapa, isipokuwa wawe wamefanya uovu ulio wazi; na kaeni nao kwa wema ; na kama mkiwachukia, basi huenda mchukie kitu na AllahAmetia heri nyingi ndani yake. (An-Nisaa 4:20)

JUZU 82 No. 235 | DH.HIJ-MUHAR.1444AH | AGOSTI 2022 | ZAHOOR 1401 HS | BEI TSH. 700/=

Ziara ya Amir imeacha alama kanda ya ziwa

Na **Mwl Abdullah Mbanga**
Redio Ahmadiyya, Mtwara

Kwa takriban siku kumi habari na mazungumzo vyote hivi huko kanda ya ziwa vilitawaliwa na ziara ya kihistoria iliyofanywa na Amir na Mubashir Mkuu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Maulana Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry aliyeongozwa na Manaibu wake wawili, Sheikh Abdulrahman Ame, Sheikh Abid Mahmood Butt, viongozi wa tanzim – Ansarullah, Khuddam, Lajna pamoja na wataalamu wa Jamaat.





Msafara huo uliongozwa na Polisi, wanajamaat waliokuwa wanajipanga barabarani kupokea ugeni huo na matangazo yaliyokuwa yanarushwa moja kwa moja na Redio Ahmadiyya chini ya Mwalim Abdullah Khamis Mbanga, uzuri uliongezeka na kuleta msisimko wa aina yake. Kwa siku hizo kumi Amir alitembelea mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Simiyu na Geita ambako alihudhuria Jalsa Salana za mikoa hiyo, kufungua misikiti, nyumba za Waalimu na kuzindua visima vya maji.

Jalsa Salana

Shinyanga

Jalsa Salana ya kwanza aliyohudhuria Amr sahib ilifanyika Shinyanga toka tarehe 28/29 mwezi wa 6/2022 hapo butibu. Jalsa Salana hii ilifana na kusisimua sana. Hotuba zilizotolewa ziliwaongezea Imani waliohudhuria akiwemo Kiongozi wa Mkoa Bi Sofia Mjema ambaye hakuficha furaha hususan kauli yetu ya Upendo kwa wote, chuki si kwa yeyote. Alieleza waliohudhuria kuwa alikuwa anaifahamu Jumuiya kwa siku nyingi na alifurahishwa na huduma zinazotolewa na Ahmadiyya kwa jamii. Na akatumia jukwaa hilo kuwahamasisha wananchi kushiriki Sensa ya watu na makazi.

Kabla ya ujaji wa Mkuu wa Mkoa, Amir sahib katika hotuba yake ya ufunguzi alieleza historia na shabaha ya Jalsa Salana. Alieleza kuwa Jalsa Salana iliasisiwa na Mashi Aliyeahidiwa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. ambaye alisisitiza katika siku hizi za Jalsa Salana waliohudhuria wamkumbue sana Allah. Katika mkutano huo mada zifuatazo ziliwasilishwa:

- Umuhimu wa Kujitolea – Sheikh Khawaja Muzaffarr – Dodoma
- Umuhimu wa Tarbiyyat na Nidhamu ya Jamaat – Sheikh Yusuf Athumani Kambaulaya
- Hotuba ya Khalifatul Masih kuhusu Utu. Hotuba hii ilisomwa na Mwalimu Ali Suleiman
- Ujio wa Imam Mahdi – Mwalim Abdus Salaam
- Umuhimu wa Kila Muislamu Kujiunga katika Jamaat Ahmadiyya - Mwalimu Abdullah Khamis Mbanga
- Kipindi cha maswali na majibu, hotuba kuhusu Utii kwa Viongozi Wote wa Kidini, Kiserikali – Sheikh A. Ame
- Mfumo wa Uongozi katika Jamaat Ahmadiyya – Sheikh Abid Mahmood Butt

Simiyu

Tarehe 01/07/2022 ilikuwa ni zamu ya mkoa wa Simiyu, Itilima. Jalsa Salana ilifana na kuhdhuriwa na Mkuu wa Wilaya Mheshimiwa Feiza Salehe. Mada zilizotolewa ni pamoja na;

- Umuhimu wa Ukhalifa – Sheikh Khawaja Muzaffar – Dodoma
- Muundo wa Jumuiya Ahmadiyya – Sheikh Abid Mahmood Butt
- Utii – Sheikh Abdulrahman Ame

Katika kufunga Jalsa Salana hiyo, Amir na Mbashiri Mkuu Maulana Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry alitoa wito kwa umuhimu wa kujitakasa kiroho



Endelea uk. 4

Mafanikio kambi za malezi Simiyu na Mara uk. 3

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

Ahmadiyya na Ustawi wa Kiswahili Tanzania

Mtizamo wa Ahmadiyya juu ya Kiswahili

Jumuiya ya Ahmadiyya inaelewa fika kuwa lugha ni neema waliyopewa binadamu ili wawasiliane na kupata shanaha ya kuumbwa kwao yaani Kumuabudu Allah. Fikra ya kwamba lugha imetengenezwa na binadamu ni potofu. sallahaAnsema katika Quran Tukufu "Na Allah Alimfundisha Adam majina yote" (2:23). Lugha kwa hiyo ni zawadi kwa binadamu kama lilivyo jua, mwezi, hew ana mengi mengineyo.

Jumuiya ya Ahmadiyya iliposajiliwa nchini mwaka 1934 ilijiwekea jukumu la kuendeleza lugha ya Kiswahili ikifahamu fika kuwa ukombozi wa kweli wa binadamu unapatikana anapokuwa na lugha yake mwenyewe ambayo ni kielelezo cha utamaduni na historia ya jamii yake.

Jumuiya ya Ahmadiyya haikuchelewa hata kidogo kuonyesha kuwa Kiswahili kina hadhi na uwezo wa kuwasilisha mawazo kwa jamii. Kabla ya ujaji wa Jumuiya ya Ahmadiyya nchini hotuba za Ijumaa misikitini zilitolewa katika lugha ambayo haikufahamika na wengi yaani Kiarabu na hotuba zenyewe zilieleza mambo ambayo hayakuwa na uhusino wa karibu na mambo yalivyo kwa hivi sasa. Masheikh wengi Afrika Mashariki walikataa kata kata juu ya uwezekano wa kutafsiri Qurani Tukufu katika lugha ya Kiswahili. Hoja yao kubwa ni kwamba Kiswahili hakina uwezo wa kubeba mawazo mazito yaliyo katika Quran Tukufu. Yote haya yalichanganyika na kasumba ya kutawaliwa. Kiswahili kilinyanyapaliwa na wale waliopata elimu ya sekondari na vyuo vikuu. Ilikuwa ni mikogo na kunata wale waliokuwa wanatafuna kimombo. Lilikuwa ni wingu zito lililowafunika wale waliokuwa wanatawaliwa.

Ilikuwa ni kazi kubwa iliyofanywa na Jumuiya ya Ahmadiyya iliyofutilia kwa mbali hoja hizo muflisi zilizokuwa zimedhamiria kubeza lugha ya Kiswahili na kuishusha hadhi mbele ya lugha nyingine. Kazi iliyofanywa na Jumuiya ya Ahmadiyya ilikuwa ni ya ukombozi wa hali ya juu. Mkoloni siku zote hukimbilia kutobanga lugha ili muweze kuidharau lugha yenu na kuenzi ile ya watawala.

Sheikh Mubarak Ahmad, Mubashir wa kwanza wa Ahmadiyya kuletwa Afrika Mashariki alipofika nchini Tanganyika alishangazwa na jambo moja Je wananchi wa nchi hii waote wanajua Kiarabu? Kama si hivyo hotuba ya Ijumaa iliyokuwa inatolewa katika Kiarabu iliwasaidiaje katika kuelewa mafundisho ya Islam!? Hotuba ya Ijumaa ina umuhimu wake katika Maisha ya Muislam. Mara moja kwa juma Waislam wa karibu na baidi wanakutana, wanajuana, wanabadiishana mawazo lakini la msingi Zaidi wanapata chakula cha kiroho ambayo ni hotuba ya Ijumaa. Hotuba ya Ijumaa ikitolewa vizuri na matayarisho ya kutosha ina uwezo wa kuathiri Maisha ya mwislam hadi siku nyingine ya Ijumaa. Hotuba ya Ijumaa inakupa kwa muhtasari yaliyojiri katika jamu na namna ya kukabiliana nayo. Shabaha yote hiyo ilipotea wakati hotuba hiyo muhimu ilipotolewa katika lugha muhimu sana katika Islam – Kiarabu, lakini haikufahamika kwa wengi.

Sheikh Mubarak Ahmad alileta mabadiliko makubwa. Kwake sala ya Ijumaa ilikuwa ni kwa wote katika jamii na wote walitakiwa wasikilize kwa makini waelewe na kuzingatia. Nia ilikuwa kwa wote ndiobaadhi. Ndio maana kwa mara ya kwanza katika historia ya nchi hii akina mama waliruhusiwa kusali msikitini wakiwa upande wao. Sheikh Mubarak Ahmad alitumia vizuri fursa hiyo ya hotuba ya Ijumaa ili kuwaonyesha wananchi kuwa Kiswahili kilikuwa na uwezo mkubwa wa kufikisha ujumbe kwa urahisi na ufasaha. Ni katika hotuba hizo za Ijumaa alipozungumzia uhuru, usawa wabinadamu, umuhimu wa elimu na kulaani maovu yaliyokuwa yanaendelea chini ya ukoloni. Hatua hii ua Sheikh Mubarak ya kutumia Kiswahili iliwaamsha wengi, kuwaelimisha wengi. Mtizamo wa Ahmadiyya juu ya lugha ya Kiswahili ulijenga mapenzi juu ya lugha hii. Mapenzi na heshima kwa lugha ya Kiswahili yakaanza kuchipuka. Haikuwa aibu au kashfa tena kusimama kadamnasi kutoa ujumbe kwa kutumia Kiswahili.

Katika miaka hiyo ya 1930 magazeti yalikuwa machache na yalikuwa machache zaidi yale yaliyotenga ukurasa kwa ajili ya mashairi. Huko alikotoka Sheikh Mubarak Ahmad zilikuwepo tayari harakati ya kuendeleza lugha ya Kiurdu na njia kubwa kule ilikuwa ni kuwahimiza washairi waandike na kazi zao zilichapishwa. Sheikh Mubarak Ahmad alitenga ukurasa maalum kwa ajili ya washairi na kuupa jina Bustani ya Washairi. Bahati nyingine iliyojitokeza tofauti na magazeti, Sheikh Mubarka Ahmad alimpata Sheikh Kaluta Amri Abedi ambaye yeye alishughulikia ukurasa hivyo na akautumia ujuzi wake wa mashairi vizuri. Bustani ya Washairi ikawavuta watunzi na washairi wa siku hizo na hivyo kuweka bayana mashairi mazuri ya Kiswahili. Watunzi wa mashairi wakapata uwanja wao, wakajuana na mwaka 1959 katika ukumbi wa Masjid Salaam Makao Makuu ya Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya ukaanzishwa Umoja wa washairi ambao ulisaidia katika kuendeleza Kiswahili, kuwarejesha watunzi kwenye mipaka inayotakiwa katika ushairi na kuchapisha Diwani za washairi. 1965 baada ya muungano baina ya Tanganyika na Zanzibar kilianzishwa Chama cha Washairi Tanzania – UKUTA Usanifu wa Kiswahili na Ushairi Tanzania. UKUTA imetoa mchango mkubwa katika kuendeleza Kiswahili.

Kama historia inavyoonyesha harakati zote hizi za kuendeleza Kiswahili zinanasibishwa kwa njia moja au nyingine na Ahmadiyya.



QUR'AN TUKUFU

وَاصْبِرْ نَفْسَكَ مَعَ الَّذِينَ يَدْعُونَ رَبَّهُم بِالْغَدَاةِ وَالْعَشِيِّ يُرِيدُونَ وَجْهَهُ ۖ وَلَا تَعْدُ عَيْنَاكَ عَنْهُمْ تُرِيدُ زِينَةَ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا ۖ وَلَا تُطِعْ مَنْ أَغْفَلْنَا قَلْبَهُ عَن ذِكْرِنَا وَاتَّبَعَ هَوَاهُ وَكَانَ أَمْرُهُ فُرُطًا

Na ujiweke pamoja na wale wanaomuomba Mola wao asubuhi na jioni, hali ya kuwa wakitaka radhi Yake. Wala macho yako yasiwaruke kwa kutaka mapambo ya maisha ya dunia. Wala usimt'ii tuliyemghafilisha moyo wake asitukumbuke, naye akafuata mata-manio yake yamepita kiasi. (Al-Kahf:29)

NUKUU YA HADITHI

حَدَّثَنَا مُحَمَّدُ بْنُ حَاتِمِ بْنِ مَيْمُونٍ حَدَّثَنَا بَهْزٌ حَدَّثَنَا وُهَيْبٌ حَدَّثَنَا سُهَيْلٌ عَنْ أَبِيهِ عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ عَنْ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ إِنَّ لِلَّهِ تَبَارَكَ وَتَعَالَى مَلَائِكَةً سَيَّارَةً فُضُلًا يَتَتَبَّعُونَ مَجَالِسَ الذِّكْرِ فَإِذَا وَجَدُوا مَجْلِسًا فِيهِ ذِكْرٌ قَعَدُوا مَعَهُمْ وَحَفَّ بَعْضُهُمْ بَعْضًا بِأَجْنِحَتِهِمْ حَتَّى يَمْلَئُوا مَا بَيْنَهُمْ وَبَيْنَ السَّمَاءِ الدُّنْيَا فَإِذَا تَفَرَّقُوا عَرَجُوا وَصَعِدُوا إِلَى السَّمَاءِ قَالَ فَيَسْأَلُهُمْ اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ وَهُوَ أَعْلَمُ بِهِمْ مِنْ أَيْنَ جِئْتُمْ فَيَقُولُونَ جِئْنَا مِنْ عِنْدِ عِبَادٍ لَكَ فِي الْأَرْضِ يُسَبِّحُونَكَ وَيُكَبِّرُونَكَ وَيُهَلِّلُونَكَ وَيَحْمَدُونَكَ وَيَسْأَلُونَكَ قَالَ وَمَاذَا يَسْأَلُونِي قَالُوا يَسْأَلُونَكَ جَنَّتَكَ قَالَ وَهَلْ رَأَوْا جَنَّتِي قَالُوا لَا أَيْ رَبِّ قَالَ فَكَيْفَ لَوْ رَأَوْا جَنَّتِي قَالُوا وَيَسْتَجِيرُونَكَ قَالَ وَمِمَّ يَسْتَجِيرُونَنِي قَالُوا مِنْ نَارِكَ يَا رَبِّ قَالَ وَهَلْ رَأَوْا نَارِي قَالُوا لَا قَالَ فَكَيْفَ لَوْ رَأَوْا نَارِي قَالُوا وَيَسْتَغْفِرُونَكَ قَالَ فَيَقُولُ قَدْ غَفَرْتُ لَهُمْ فَأَعْطَيْتُهُمْ مَا سَأَلُوا وَأَجَرْتُهُمْ مِمَّا اسْتَجَارُوا قَالَ فَيَقُولُونَ رَبِّ فِيهِمْ فُلَانٌ عَبْدٌ خَطَّاءٌ إِنَّمَا مَرَّ فَجَلَسَ مَعَهُمْ قَالَ فَيَقُولُ وَلَهُ غَفَرْتُ هُمْ الْقَوْمُ لَا يَشْقَى بِهِمْ جَلِيسُهُمْ

Tafsiri: Abu Huraira (RA) anasimulia ya kuwa : Mtume (SAW) alisema : Mwenyezi Mungu ana Malaika ambao hutembea mitaani wakiwatafuta wanaojishughulisha na kumkumbuka Mwenyezi Mungu na wanapoikuta jamii ya watu wakijishughulisha na dhikri ya Mwenyezi Mungu. Malaika hawa wanakaa nao na huwafunika watu hao kwa mabawa zao wakipangana hadi mbinguni. Basi Wanapo tawanyika watu hawa, Malaika hupanda mbinguni na hapo Mwenyezi Mungu Mola wao huwauliza: Mmetoka wapi? Nao watasema, tumetoka kwa watu wako, wanaokutukuza na kukuadhimisha na kukusifu na kukuuliza. Atawauliza Malaika, wanaomba nini? Watajibu, wanakuomba Pepo yako. Atasema (Allah Mtukufu) Je wao waneiona ? watajibu: La, Wallahi, hawajaiona! Basi Atasema (Mungu): Ingekuwaje kama wangeiona? Watasema Malaika: Wanakuomba walindwe. Mola Atawauliza: wanaomba kulindwa na kitu gani? Watajibu: kulindwa na moto wako! Atauliza: Je wameuona moto wangu ? Watajibu: Hawajauona. Atawaambia Je wangeuona wangekuaje? Watasema nao wanakuomba msamaha pia, Hapo Mwenyezi Mungu Atawaambia : Nimekwisha wasamehe wote na nimekwisha wapa waliyoomba na Nimewapa ulinzi na kile walichokiomba kulindwa nacho. Malaika watasema: Ee Mola wetu! Ndani yao kuna mwenye hatia ambaye alipita hapo na akakaa pamoja nao. Mwenyezi Mungu atajibu : Yeye pia nimemsamehe,kwani hao ni watu ambao mwenye kukaa nao hawezi kuwa na bahati mbaya.(Sahih Muslim)

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Dr. Swaleh Kitabu Pazi
Kompyuta: Ahmad Abdul Nasibu.
Mchapishaji: Sheikh Raghib Zia ul Haq
Msambazaji: Mwl. Omari Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Mahmood Hamsin Mubiru.
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu36@gmail.com

Mafanikio ya kambi za malezi Mkoani Simiyu na Mara

Ali Dino Tahir (Sheikh wa Mikoa wa Simiyu na Mara):

Kwa fadhila za Allah Mtukufu na Baraka zake tele alizozitupatia sisi waislamu Ahmadiyya Mhe.Amir Sahib na Mbashiri Mkuu Tanzania alipotutembelea mkoni Simiyu na kutuhimiza kuhusu Malezi ya watoto . Kulitekeleza agizo lake tulianza kazi mara moja. Toka Julai 2021 hadi June 2022 katika Mkoa wa Simiyu na Mkoa Jirani Mkoa wa Mara tulifanya Kambi za Malezi au Tarbiyyati Classes zisizopungua 15. na Mkoa wa Simiyu katika kila kambi idadi ya wanafunzi ilikuwa 200 mpaka 280. Kwa sasa katika kila tawi tunao Maimamu wa kutosha tunawaita Maustadhi au waalimu wadogo wanaojua Sala na Tafsiri neno kwa neno na kuwafundisha watoto wengine bila ya kuangalia dini wala kabila hata wasio na dini wanawasomesha tu. Na Hao Maustadhi wadogo wanaweza kusalisha Sala vizuri na wengine huwa wanatoa Hutuba za Ijumaa katika matawi yao ikiwa hakuna mwalimu au Sheikh na badhi ya wakati hata mbele yao huwa wanatoa hutuba. Alhamulillah ala zalika

Katika Mikoa yetu Simiyu na Mara Atfal ul Ahmadiyya na Khudamul Ahmadiyya pamoja na Nasirat ul Ahmadiyya na Lajna Imaillah wasiopungua 300 walishahifadhi Sala na Tafsiri neno kwa neno na wanasoma maswali na majibu ya dini na kuwafundisha marafiki, majirani na ndugu zao.

Miongoni mwao wapo waliomaliza Maswali na majibu zaidi ya 1150 na walishamaliza kusoma vitabu ya dini kama Mhisani kwa binaadamu na Upendo wa Mtume Muhammad SAW kwa watoto. Mtoto mmoja alikisoma kitabu hiki mara 11. Wengine mara saba mara tano n.k ukiwauliza swali lolote kupitia vitabu vile watakujibu vizuri tu

Na katika makambi Sheikh Sahib huwa anawauliza maswali na majibu wakiwa wanajibu ana kwa ana na kwa makini kiasi kwamba akichelewa mwanafunzi sekonde tatu tu ameshakosa,na katika mitihani huwa wanafaulu kwa kushangaza. Na ukiandika katika youtube ATFAL WA SIMIYU au NASIRAT WA SIMIYU utaweza kuwaona jitihada zao kupitia simu yako janja au compyuta

Katika makambi tuwasikilizisha Hutuba za Khalifa mtukufu Ayadahullahu binassirihilaziz na waalimu wote huwa wanasikiliza nao na kuandika maswali 35 mpaka 40 kupitia ile hutuba wanayosikiliza mara moja tu,wakiulizwa Maswali kupitia ile hutuba,Atfal ,Khudam na Nasirat wa Simiyu ni adimu kukosa jibu . Ukitaka kuwasikiliza andika maneno haya katika Google au Youtube {Mfano bora kuisikiliza Hutuba ya Khalifa mtukufu} utawaona wanapojibu.

Majina ya Atfal Na Khudam waliopata nafasi katika kusoma Orodha ya Atfal na Khudam 10 waliohifadhi maswali mengi

1. Muhammad Sasa Tawi la Kisesa (Maswali na majibu ya dini 1168)
2. Tariki Omari Tawi La Ntobo (Maswali na majibu ya dini 1068)
3. Salim Mange Tawi la Ntobo (Maswali na majibu ya dini 1038)
4. Nasri Doto Tawi la Ntobo (Maswali na majibu ya dini 1030)
5. Yahya Dida Tawi la Ntobo (Maswali na majibu ya dini 929)
6. Ibrahim Doto Tawi la Ntobo (Maswali na majibu ya dini 920)
7. Shabani Abubakari Tawi la Ntobo (Maswali na majibu ya dini 832)
8. Hamisi ndakama Tawi la Ntobo (Maswali na majibu ya dini 800)
9. Mubarak Emanuel Tawi la Nyangokolwa (Maswali na Majibu 750)
10. Musa Njile Tawi la Nangale (Maswali na Majibu 625)
11. Farid Ibrahim Tawi la Kisesa (Maswali na majibu ya dini 600)
12. Shabani Mohammadi Tawi la Mitobo (Maswali na Majibu ya dini 560)
13. Abdallah Habibu Tawi la Kisesa (Maswali na majibu ya dini 510)

N.B: Wapo Atfal na Khudam mamia wengine wanaohifadhi maswali chini ya idadi hii hawajaorodheshwa hapa

Waliosoma kitabu Mhisani kwa Binaadamu na kufuzu mtihani

1 Muhammad Sasa Tawi la Kisesa
2 Tariki Omari Tawi La Ntobo
3 Salim Mange Tawi la Ntobo
4 Nasri Doto Tawi la Ntobo
5 Yahya Dida Tawi la Ntobo
6 Shabani Abubakari Tawi la Ntobo
7 Ibrahim Doto Tawi la Ntobo
8 Hamisi ndakama Tawi la Ntobo
9 Farid Ibrahim Tawi la Kisesa
10 Abdallah Habibu Tawi la Kisesa
11 Juma Masanja Tawi la Kisesa
12 Tatu Ibrahim Tawi la Kisesa

Majina ya Khudam na Atfal ambao ni Maimamu na idadi ya wanafunzi wao:

1. Mohammad sasa Tawi la Kisesa anasomesha wanafunzi 57
2. Abdallah Habibu Tawi la Kisesa anasomesha wanafunzi 50
3. Chakwanza Rashidi Tawi la Nyamuswa Mkoa wa Mara. Anafundisha wanafunzi 43
4. Issa Musa Tawi la Gambasingu anasomesha wanafunzi 37
5. Ally Razaro Tawi la Mwaukoli anasomesha wanafunzi 30
6. Anjum Sid Tawi la Gambasingu anasomesha wanafunzi 20
7. Mohammad Nyeleja Tawi la Mwaukoli anasomesha wanafunzi 15
8. Husain Iddi Tawi la Gambasingu anasomesha wanafunzi 12
9. Amosa Altaba Tawi la Gambasingu anasomesha wanafunzi 11
10. Nshoma Maduhu Tawi la Gambasingu anasomesha wanafunzi 11
11. Salim Mange Tawi la Ntobo anao wanafunzi 10
12. Juma Masanja Tawi la Kisesa anawafundisha watoto 10
13. Mwasi Mohammad Tawi la Gambasingu anasomesha wanafunzi 10
14. Horo Sosoma Tawi la Gambasingu anasomesha wanafunzi 10

N.B.: Wengine wapo wengi sana wanaosomesha wanafunzi chini ya idadi hii amabo hawajaadikwa hapa

Majina ya Nasirat wanaowasomesha kama waalimu

1. Ashura Kiumbi Tawi la Ntobo amehifadhi maswali 200 na anafundisha wanafunzi 4
2. Nasirat Paulo Tawi la Ntobo amehifadhi maswali 105 na anafundisha wanafunzi 3
3. Khadija Ibrahim Tawi la Kisesa anafundisha wanafunzi 15
4. Halima Buyamba Jamaat ya Mwaukoli anafundisha wanafunzi 12
5. Khadija Nkali Tawi la Kisesa anafundisha wanafunzi 10

N.B: Wapo Nasirat wengine wengi wanaosomesha chini ya idadi hii hawajaorodheshwa hapo

Matawi Bora katika Malezi

Katika mikoa yetu Simiyu na Mara kati ya matawi 56; Tawi namba moja katika mkoa wa Simiyu na Mara upande wa Malezi ni Tawi la Ntobo. Ndani ya tawi hili kuna Atfal na Khudam wetu saba waliomaliza kuyahifadhi maswali zaidi ya 800. kati ya Vijana hao watatu ni wale waliomaliza zaidi ya maswali 1000.Hatuna mwalimu wa jamaat katika tawi hili, vijana wanasomeshana wenyewe kwa wenyewe ,na kuchukua nafasi kwa wingi katika mashindao.

Tawi Bora namba mbili ni Tawi la Gambasingu , hapa pia Hatuna Mwalimu wala msikiti , mtoto mmoja anayeitwa Issa Musa anayesoma darasa la nne alianzisha kuwasomesha watoto kabla ya mwaka sasa watoto wengi aliowasomesha yeye,ni waalimu wadogo mitaani na wanao wanafunzi wengi,hawa waalimu wadogo wana jadhba kubwa kiasi kwamba hawazuiliwi na mvua ,jua ,njaa wala kiu wanasoma kila siku chini ya miti,nyumba za watu ,wakati wa kwenda shule na kurudi,hakuna fursa wanaoacha. Tawi hili linasimamiwa na Mwl Idi Sembe wa Kisesa

Tawi la tatu ni Tawi la Mwabuma. Tawi hili linasimamiwa na Mwl Kasim Kimwaga. Mwlimu huyu alitoka Jamia Ahmadiyya Tanzania mwaka huu mwanzoni lakini ijitihada zake ni kubwa sana amelibadli tawi la Mwabuma na Wanafunzi wake

Tawi la Nyamuswa (Mkoa wa Mara)

Katika Mkoa wa Jirani yaani Mkoa wa Mara Tawi ambalo limejitahidi sana katika miezi hii sita walipoungana nasi ni Tawi la Nyamuswa , Tawi hili linasimamiwa na Mwl. Zulkher said Kapite.

Waalimu Bora katika Mikoa wa Simiyu na Mara.

Namba Moja ni Mwl Iddi Sembe. Wanafunzi wake wengi wanasomeshana wenyewe kwa wenyewe. Katika Matawi yake kuna makambi ya Malezi kila siku wanaoendesha watoto wenyewe kwa wenyewe chini ya miti wengine wanasomeshana machungani. Ukitembelea Matawi yake utaona watoto wanasomeshana katika nyumba za watu,mitaani nk.Mwlimu Idi sembe anawatembela sana anawasimamia na kuwahoji walifikia wapi na kuwahimiza sana ,matokeo yake vijiji vyake vyote vimevamiwa na waalimu wadogo Atfal na Nasirat

Maisha ya Mtume Muhammad saw



Yalivyosimuliwa na Hadhrat Mirza Bashir ud Din Mahmud Ahmad^{ra} Khalifatul Masih wa pili wa Masihi Aliyeahidiwa^{as}

Inaendelea Kutoka toleo lililopita

NJAMA ZA WATU WA MAKKA ZA KUWASUMBUA TENA WAISLAMU

Baada ya kupita miezi miwili mitatu hivi, mfadhaiko wa watu wa Makka ukaondoka nao wakaanza tena kuwazia mipango ya kuwasumbua tena waislamu. Lakini baada ya kushauriana wakahisi kwamba kuwasumbua tu wale waislamu walioko makka na pembezoni mwake hawataweza kufanikiwa katika makusudio yao. Wao wataweza tu kuufuta Uislamu watakapomuondosha Mtume s.a.w. huko Madina. Hivyo baada ya kushauriana hivi, watu wa Makka wakamuandikia barua Abdullah bin Ubayy bin Salul, ambaye kuhusiana naye ilikwisha elezwa hapo awali kwamba kabla ya ujio wa Mtume s.a.w., watu wa Madina walikuwa wameshaamua kumfanya yeye kuwa mfalme wao, na kumuelekeza kwamba watu wa Makka wamechukizwa sana kutokana na kuhamia Madina kwa Mtume s.a.w., Watu wa Madina hawakupaswa kumpa yeye na wenzake makimbilio. Mwishoni kulikuwa na maneno haya:

Sasa kwa kuwa ninyi mmempa kimbilio Muhammad s.a.w., basi tunatangaza hivi kwa kula kiapo cha Mwenyezi Mungu kwamba aidha ninyi watu wa Madina mpigane vita mkishirikiana naye au mumfukuze kutoka kwenye mji wenu, waila sisi sote tutajumuika na kuishambulia Madina na tutawaua watu wote wa Madina wenye uwezo wa kupigana vita na kuwafanya watumwa wanawake wenu

Kupatikana kwa barua hii kukaifanya nia ya Abdullah bin Ubbay bin Salul iharibike kidogo naye akashauriana na wanafiki wengine kwamba; 'kama tutamruhusu Muhammad, mtume wa Allah s.a.w. kuishi hapa, basi mlango wa hatari mbali mbali kwetu utafunguka, hivyo yatupasa sisi tupambane naye vitani na kuwafurahisha watu wa Makka.

Mtume s.a.w. akapata taarifa ya jambo hili na akaenda kwa Abdullah bin Ubayy bin Salul na kumfahamisha kwa kumwambia: 'Kitendo chako hiki kitakuwa ni chenye madhara kwako mwenyewe, kwa sababu wewe wafahamu kwamba watu wengi wa Madina wameshakuwa Waislamu nao wako tayari kuyatoa muhanga maisha yao kwa ajili ya Islam. Ikiwa mtafanya hivyo, basi watu hao, kwa yakini kabisa, wataungana na wahamiaji, nanyi, baada ya kuianzisha vita hii, mtaangamia kabisa.' Abdullah bin Ubayy bin Salul akalitambua kosa lake na akajiepusha na dhamira hii.

MKATABA WA UNDUGU KATI YA WAISLAMU WALIOHAMIA MADINA TOKA MAKKA (MUHAJIRIIN) NA WAISLAMU WENYEJI WA MADINA (ANSWAR)

Ndani ya siku hizo hizo Mtume s.a.w. akatengeneza mpango mwingine kwa ajili ya kuiimarisha Islam, nao ni huu kwamba aliwakusanya Waislamu wote na kuwafanya wawili wawili (mmoja miongoni mwa Ansar na mwingine miongoni mwa wahamiaji) wawe ndugu.

Waislamu wa Madina waliukaribisha mkataba huu wa undugu kwa dhati ya moyo kiasi hiki kwamba waliwachukua ndugu zao wa mkataba na kuwapeleka majumbani mwao na kuweka mbele yao mali zao zote wakiwaambia wazigawe mali hizo nusu kwa nusu. mwislamu mmoja miongoni mwa Ansar alifikia hatua hii kwamba alimsisitizia ndugu yake akimwambia 'Mimi namtaliki mmoja kati ya wake zangu ili upate kumuoa.' Lakini Wahaajir wakatoa shukrani ya uaminifu wao huu na kuzikataa hadia hizo za kuchukua hisa yoyote katika mali zao. Lakini juu ya hayo, Answar wakasisitiza na kumwambia hivi Mtume s.a.w. 'Ewe Mtume wa Allah! Wakati hawa Wahaajir wameshakuwa ni ndugu zetu, sasa yawezekanaje wasiwe na hisa katika mali zetu? Naam, kwa kuwa hawa ni wafanya biashara wasio na uzoefu na ukulima, basi kama hawachukui hisa katika mashamba yetu, angalau wafanywe wawe wenye hisa katika mazao yale yanayovunwa humo. Wahaajir bado wakawa hawako tayari kuchukua hisa hata katika haya (mazao) na wakajiingiza kwenye fani ya mababu zao ya biashara na baadhi yao wakawa wenye mali nyingi ndani ya siku chache tu.

Lakini Ma Answar walisisitiza sana katika kuitoa hisa hiyo kiasi ya kwamba baadhi ya Ma Answar walipofariki, watoto wao, sawa na mila za waarabu, wakawapa hisa ndugu zao wahamiaji kutoka katika mali ya marehemu na ikaendelea kutendeka hivi kwa miaka mingi hadi ilipoteremka ndani ya Kurani Tukufu amri ya kuifuta amali hii.

Ziara ya Amir yaacha alama Kanda ya ziwa





na kuitafuta taqwa. Taqwa ndio mzizi wa mema yote.

Geita

Kwenye kijiji cha Nungwi tarehe 04/07/2022 mkoani Geita Jalsa Salana ilianza na hotuba za kuongeza Imani zilizotolewa;

- Mwalimu Najat Fakim alizungumzia Bishara ya Ujaji wa Masihi Aliyeahidiwa
- Alivyosema Masihi Aliyeahidiwa – Mwalimu Ramadhani Mkieti
- Ubora wa Mafundisho ya Islam – Mwalimu Ramadhan Mahmood
- Utii kwa Wenye Madaraka – Sheikh Abdulrahman Ame

Kutokana na majukumu mengine, Mkuu wa Mkoa hakuweza kuhudhuria isipokuwa aliwakilishwa na Afisa Elimu wa Mkoa Bwana Anthony Mtweve ambaye alipongeza kazi nzuri inayofanywa na Jamaat Ahmadiyya katika kuihudumia jamii.

Baada ya salamu hizo kutoka kwa Mwakilishi wa Mkuu wa Mkoa utoaji wa mada uliendelea.

- Nidhamu ya Jamat Ahmadiyya – Sheikh Abid Mahmood Butt
- Umuhimu wa Ukhalifa – Sheikh Khawaja Muzaffar

Sheikh wa Mkoa, Sheikh Ehtisham alieleza maendeleo ya Jamaat na juhudi za kufikisha ujumbe wa Masihi Aliyeahidiwa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad^{as}. Alieleza pia Jamaat Ahmadiyya imejenga misikiti 8 na nyumba za Waalimu. Mwaka huu wamejiunga watu 2110 hivyo mkoani kuna wanajamaat 4870.

Akifunga Jalsa Salana, Amir sahib aliwataka waaminio kuhudhuria msikitini na kutafuta kwa udi na uvumba elimu ya dini.

Kufungua msikiti



Kanda ya ziwa imejiongezea misikiti kutokana na ziara ya Amir sahib. Misikiti ifuatayo ilifunguliwa:

Masjid Fatih – Ushetu – Shinyanga
Masjid Masroor – Bukomile
Masjid Fazl – Itilima – Simiyu
Masjid Furqaan – Kantaange – Chato, Geita
Masjid Tahir – Kitigiri – Geita

Na nyumba zifuatazo za Waalimu zilifunguliwa:

Kageye – Geita Vijijini
Mwamala – Kijiji
Shabuluba
Nhumbili
Wigehe – Kahama
Masjid Fazl – Nyumba ya Mwalimu

Kiswahili - Toka jana hadi leo



Na

Mwl Abdullah Hamis Mbanga,

Redio Ahmadiyya,

Mtwara

Mwandishi mashuhuri wa historia ya Kiswahili Jan Knappert alipopewa jukumu la kuandika *Historia ya Ushairi wa Kiswahili* na Shirika la Heinemann mnamo mwaka 1969 alionekana kufurahi aheshima hiyo. Alidhani kuwa ingekuwa ni kazi rahisi mno kwake. Mara moja alianza kukusanya baadhi ya maelezo hayo aliyakusanya kutoka Afrika ya Mashariki na hasa Kenya na Tanzania tangu mwaka 1953.

Kwa uchache alikadiri kuwa kazi hiyo ingemchukua muda usiozidi fungate moja la miaka (miaka 7). Hatimaye alibaini kuwa kazi hiyo si rahisi kiasi hicho, na alikiri kuwa historia ya Kiswahili si tu haijapata kuandikwa bali haitapata kuandikwa. Kwa maana habari zake ni adimu mno, nyaraka kuhusu historia yake zilizohifadhiwa kwa bahati ni chache mno.

Hadi mwaka 1979 alipotoa chapa ya kwanza ya kitabu *Charlie Four Centuries of Swahili Verse* bado usiri wa habari za tarehe ya Kiswahili na Waswahili uliendelea kumtindika.

Hali kama iliyomkuya Jan Knappert, ndiyo ada imkutayo mtafiti yeyote wa tarehe ya Kiswahili au ya waswahili.

Pamoja na kuwa Kiswahili ni miongoni mwa lugha kuu na kongwe, lakini bahati mbaya ni kwamba haikupata tazamo la haiba kutoka kwa watumizi wake. Haieleweki ni kwa nini lakini huu ni ukweli ulio wazi. Ingawa kiumri, Kiswahili ni kikubwa kuliko Ki-urdu na kimalai, lakini ndiyo lugha yenye kazi chache mno za kiandishi. Huenda shirika la Heineman linastahili kushukuriwa na waswahili kwa kumshawishi mswahili mweupe Jan Knappert kudodosa na kuamsha angalau Tarehe ya ushairi wa Kiswahili.

Inadaiwa kuwa moja ya sababu zinazotajwa kwa Kiswahili kukosa haiba katika jamii ya wasoma lugha wa kimataifa ni kule kudhaniwa kuwa huenda ni lugha chotara, wakimaanisha kuwa ni nusu Kiarabu na nusu Kibantu.

Kasumba hii kwa bahati mbaya ilipenya hata katika nyoyo za waswahili waliodhaniwa kuwa wameendelea. Walianza kutukuza lugha za kigeni, hasa zile za wakoloni wao, wakakiacha Kiswahili kikienziwa na makabwela tu, wavuvi na watu wa masokoni, hata hatimaye Kiswahili katika baadhi ya miji kilijulikana kama 'kisokoni' yaani ni lugha kwa ajili ya watu wa mitaani wa hali ya chini. Na hivyo ikahesabiwa kuwa si lugha ya kielimu na kimaendeleo.

Kiswahili mwanzoni kiliandikwa kwa herufi za Kiarabu. Inaaminika kuwa hata manju wakubwa wa karne nane za mwanzo katika tarehe ya Kiswahili aghalabu walikuwa ni masheikh wa Kiislam. Kwa wakati huo Kiswahili, kama ilivyokuwa kwa Ki-urdu katika India, kilihesabika kuwa ni lugha ya Waislam. Maana wasomi wote wa Kiswahili walilazimika kwanza kusoma alif, bee, tee za Kiarabu ndipo waweze kusoma na kuandika Kiswahili.

Tatizo hili la kuwa lugha chotara, jambo kubwa lililowachusha wengi kukizamia Kiswahili, kkwani Knappert anataja sababu nyingine kubwa iliyochangia wasoma lugha hasa wale wa kimagharibi kukosa hamasa ya kukizamia Kiswahili.

Tatizo lenyewe ni hili ya kwamba waandishi waote wa mashairi na tenzi na Kiswahiil kuanzia mwaka 1650 hadi 1850 walikuwa ni Waislamu. Mashairi yote waliyoandika aghalabu yalikuwa ni mawaidha ya kidini na sifa za Mtume wao mtukufu. Hili liliwavunja nguvu wasomi wa kimagharibi kuzamia katika fasihi ya Kiswahili, kwa maana walilazimika kuwa na ufahamu mkubwa wa imani hiyo ndipo waweze kuendana na maelezo ya washairi hao. Hivyo walijikuta wakisoma Islam zaidi kuliko fasihi ya lugha.

Ni kweli kabisa kwa wakati huo haikuwa rahisi kutofautisha uswahili na Uislamu. Lakini hii pia si hoja inayofaa sana, kwa kuwa hata hao waswahili manaizi wa enzi hizo ambao walikuwa ni waislamu waliendelea kutukuza Kiarabu badala ya Kiswahili. Hata ile dhana ya kuwa Kiswahili ni pijini ya Kiarabu – Kibantu ilizaliwa wakati huo ambapo watu wenye kujipata katika jamii walikuwa wakiongea kwa jinsi ya baadhi ya wasomi wa leo wanavyozungumza Kiswa-Kinge, badala ya mbona ume-late (umechelewa) enzi hizo ilitamkwa umeta-akhari, na hii ilifanyika kwa kasumba ile ile ya mtu kutaka kuonyesha angalau ameelimika.

Kwa hivi Kiswahili kilianza kudharauliwa tangu mwanzoni mwa historia yake. Kwani katika zama hizo Islam ndiyo ilikuwa kama dini kuu katika maeneo ya uswahilini. Hata hivyo viongozi wa kidini wa enzi hizo, hawakuwa tayari kukitumia Kiswahili kutafsiri aya za Kur-ani Tukufu. Hata hotuba za Ijumaa zilitolewa kwa lugha ya Kiarabu.

Kuna ushahidi kwamba wapo baadhi ya Masheikh waliohubiri kwamba lugha yetu sio tu haijitoshelezi bali pia ni najisi kuitumia kwa kufasiri maneno matakatifu ya Mungu. Hapa tunaona kwamba ingawa Kiswahili kilionekana kama lugha ya Waislam, lakini hata katika zama hizo za mafanikio ya Islam bado Kiswahili kilibezwa hata na viongozi wa Kiislam. Inawezekana kabisa kwamba hii ilikuwa ni hali ya kutojiamini kutokana na kutawaliwa. Iliwafikisha watu hadi katika hali ya kudhani kuwa hata lugha yao haitoshi kuwakilisha mada nzito za kielimu kama vile za dini. Utando wa kasumba hiyo unapatikana hata sasa miongoni mwa waswahili ambapo hata maneno ambayo hupatikana kwa namna anuwai katika lugha yao mama wao hudiriki kujikanyaga na kutafuta ya Kiingereza.

Hii yote ni ile hali ya ushamba wa kielimu kuchanganya lugha mbili hata kama anazungumza na watu ambao ana hakika ya kwamba si wajuzi wa lugha ngeni.

Tatizo jingine la kuadimika kwa uwepo wa maandiko yanayhusu historia ya Kiswahili na waswahili maarufu ni la kijiografia. Ingawa katika watu waishio katika Afrika ya kitropiki ni waswahili pekee ndio walioanza kuendeleza uandishi wa fasihi zao. Lakini kwa bahati mbaya waswahili walio katika ukanda wenye unyevunyevu na mvua nyingi wa sayari hii, mbali na kuwa na mazingira ya joto na unyevunyevu, kuna maadui wengi wengine wa karatasi: mchwa, mende, na mvua zisizotabirika.

Kutokana na nyenzo hizo za uharibifu, inadaiwa kuwa ni nusus dazanitu au zaidi ya miswada ya maandiko ya Kiswahili iliyoandikwa Kabla ya mwaka 1800 iliyomudu kubaki bila kuharibika. Kwa hali hii inawezekana kabisa ya kuwa baadhi ya sira za manju na maisha ya baadhi ya wafalme ziliandikwa, lakini zikateketea kutokana na athari hizo za kijiografia.

Tofauti na Ulaya, mashariki ya kati, Afrika ya kaskazini, kaskazini mwa India na China, miswada ilidumu makumbushoni na kutufikia. Hata katika mabaki ya kale yaliyogunduliwa baadaye katika maeneo hayo, nyaraka juu ya maisha ya waandishi mashuhuri, barua zao, mashairi yao, mikataba ya kale, takwimu za mapato na matumizi, ziligunduliwa na kufanya safari ya utambuzi wa historia ya lugha na tamaduni zao kuwa isiyokwama.

Lakini kwa upande wa Kiswahili, bahati kama hiyo imekosekana. Na hata baadhi ya byaraka chache zilizookoka kibahati katika uharibifu huo ni zile ambazo hazipo katika mikono ya Waswahili wenyewe. Kuna barua chache na nyaraka nyingine zihusuzo mawasiliano ya kidiplomasia baina ya Ureno na Pate ambazo zimehifadhiwa katika makumbusho ya mjini Lisbon:

Labda bahati ndogo tuliyonayo waswahili ni angalau kukumbuka kwa ghaibu baadhi ya tenzi, mashairi na majina ya baadhi ya manju maarufu wa zama za mwanzo: Aidarusi, Bwana mwengo na mwanawe Abu Bakari, Muyaka bin Jaji Al Ghasani, Fumo Liongo na wachache wengine.

Hata hivyo ni vigumu kujua waliishi lini na wapi. Tunakadiria zama za maisha yao kuwa kwa kubahatisha tu, na tunakisia maeneo yao ya kuishi kuwa ni eneo la pwani ya Afrika Mashariki ambapo kitovu chake kilikuwa ni katika visiwa vilivyo pwani ya Kenya hatujui zaidi ya hapo.

Kwamba walizaliwa tarehe ipi na kufariki lini, ni swali lisilo na majibu katika tarehe yetu. Hata kaburi la Muyaka ambaye inahisiwa huenda alifariki mnamo mwaka 1837 haijulikani lilipo. Kaburi la Fumo Liongo linadhaniwa kuwa ni lile lililopo karibu na mto Ozi, lakini ni vigumu kwa mtu kuamini kuwa kaburi hilo lenye urefu wa futi kumi na mbili ni la mwanadamu.

Hatufahamu chochote kuhusu asili za waandishi hao. Ikiwa wazazi wao walikuwa matajiri au masikini. Ni Muyaka pekee ndiye ambaye angalau anaweza kuwa mshairi wa kwanza wa Kiswahili ambaye tunaweza kubabaisha maelezo juu ya maisha yake. Na hii ni kutokana na baadhi ya tungo alizoandika kuhifadhiwa fuadini na wafuasi wake. Lakini hakuna maandiko yoyote ya historia yake

Endelea uk 9

Bustani ya Washairi

AHMADIYYA NA MAENDELEO YA KISWAHILI – TANZANIA

Na **Mahmood Hamsin Mubiru**

Inaendelea Kutoka toleo lililopita

Sheikh Mubarak....

106. Watunzi wa mashairi,
Kiswahili ni bahari,
Bahari ilo shwari,
Popote waogelea.

107. Na watoaji hotuba,
Kiswahili mahabuba,
Hilo pengo kinaziba,
Watu kuwatumikia.

108. Waandikaji wa insha,
Zinazohusu maisha,
Lengo kukamilisha,
Kiswahili kimetua.

109. Twakipenda Kiswahili,
Lugha yetu ya asili,
Tamu mithili asali,
Pole msiyoijua.

110. Ni tamu kwa matamshi,
Lugha hino ya aushi,
Katu kwetu haichoshi,
Hatuchoki kutumia.

111. Lugha hino muujiza,
Tena bila kutangaza,
Au watu kuumiza,
Baidi imeenea.

112. Bila ya kuwa na dola,
Imefanya makabila,
Tukapata moja mila,
Ambayo twajivunia.

113. Ni mila ya Kiswahili,
Ilo tupa ukamili,
Tukaipata akili,
Ya kujenga Tanzania.

114. Ni lugha ya ukombozi,
Kuwapinga walowezi,
Lugha inafanya kazi,
Wanyonge kujitambua.

115. Ndiyo lugha ya wanyonge,
Daima wasaka tonge,
Kutwa shamba la mkonge,
Kidogo kuambulia.

116. Kiswahili ni tajiri,
Nahau na mashairi,
Ni lugha yenye hadhari,
Heshima yahitajia.

117. Lugha inao utamu,
Kusema hawishi hamu,
Inafaa kwa elimu,
Watoto kufundishia.

118. Sio lugha ya kabila,
Na hivyo haina hila,
Eti ya makabaila,
Mbona sote twatumia.

119. Na hata bila kitali,
Wa hapa hata wa mbali,
Wakinena Kiswahili,
Na huku wametulia.

120. Kusema na kuandika,
Lugha imekamilika,
Ni nzuri haina shaka,
Rahisi kuitumia.

121. Hadithi pamwe methali,
Ni nzito sio sahali,
Imejaza nyingi mali,
Ukitaka watumia.

122. Hayo ni yake maoni,
Sheikh wetu Shabaluni,
Mubaraka muhisani,
Kandili katuwashia.

123. Si maneno kwa vitendo,
Akauleta uhondo,
Akabadili mwenendo,
Kiswahili kutumia.

124. Vitendo vina ujumbe,
Vitamu mithili embe,
Vitendo hasa ni jembe,
Shamba ukajilimia.

125. Kaonesha kwa mifano,
Kiswahili ni mswano,
Kinaleta muungano,
Kivuli kutuletea.

126. Hizo zama za awali,
Kabla hajawasili,
Marufuku kiswahili,
Hotuba ya ijumaa.

127. Lugha iliyo twayibu,
Ilikuwa Kiarabu,
Kiswahili ni aibu,
Watu kuwahutubia.

Si maneno ni vitendo.

128. Ni ulama wa vitendo,
Huo ndio wake mwendo,
Kwa huo wake mtindo,
Mengi akatufanyia.

129. Hotuba akabadili,
Kutumia kiswahili,
Uamuzi wa asali,
Hotuba za ijumaa.

130. Kutumia kiswahili,
Kuufikisha ukweli,
Palinoga kwelikweli,
Kiswahili kusikia.

131. Ilikuwa ni tamasha,
Ujasili kaonesha,
Kwamba lugha ya maisha,
Ni hii kuitumia.

132. Kwamba lugha ilo hai,
Hapa chini ya samai,
Kwa sisi tulio hoi,
Ni kiswahili tambua.

133. Ipeni sana heshima,
Hino ndiyo lugha mama,
Kutupa sisi uzima,
Maisha kuendelea.

134. Urithi huno faradhi,
Kwa sisi kutupa hadhi,
Ushike huno waadhi,
Nchi itaendelea.

135. Itunze mboni ya jicho,
Utaweza ona hicho,
Na mengineyo kwa macho,
Utaweza jionea.

136. Kila lugha ina miko,
Inalo lake zindiko,
Hayo tuyape ujiko,
Lugha ipate chanua.

137. Kazi ile ya heshima,
Ya kitabu cha Karima,
Kwa bidii kainama,
Kaanza tufasiria.

Kurani Tukufu kwa Kiswahili.

Utaendelea toleo Lijalo

NDOA SI NDOANA

Yailahi Ya Jalali, niongoze hii njia
Ili niseme ukweli, kwa yale yalo sawa
Mana ni njia ya kweli, tukishika sawia
Kumbe ndoa si ndoana, ni sehemu ya furaha

Ndoa ni sehemu yetu, na nusu ya dini yetu
Kasema Mtume wetu, hatuwezi kata katu
Yeye ni kigezo chetu, tena ndio bwana wetu
Kumbe ndoa si ndoana, ni sehemu ya furaha

Kuita ndoa ni pingu, utakuwa wakosea
Utaitia ukungu, na kuleta mazoea
Mwisho utaona chungu, utake kuikimbia
Kumbe ndoa si ndoana, ni sehemu ya furaha

Usije kudai haki, bila wajibu kujua
Usome kitabu hiki, Qur'ani nakwambia
Mana hutoleta chiki, kama ukiitambua
Kumbe ndoa si ndoana, ni sehemu ya furaha

Ni vyema usome kwanza, ujue wajibu wako
Ili ukawe wa kwanza, kuutekeleza huko
Hata huyo wako mwenza, nae atakupa heko
Kumbe ndoa si ndoana, ni sehemu ya furaha

Salma Kachima mwalimu, ametukumbusha sana
Ili tukaishi humu, tukiwa twatulizana
Wala isitwishe hamu, ya sisi kushikamana
Kumbe ndoa si ndoana, ni sehemu ya furaha

Dada etu Mama Pazi, akasema neno moja
Twende tukawe wawazi, tutengeneze umoja
Tusiwe mapaparazi, tutengeneze vioja
Kumbe ndoa si ndoana, ni sehemu ya furaha

Ukiwa we mfalme, akawe ye malikia
Wala usiwe kangome, ya yeye kukwangukia
Umpongeze kwa shime, pale atapopatia
Kumbe ndoa si ndoana, ni sehemu ya furaha

Misukosuko ya ndoa, ni sehemu ya Maisha
Ni wajibu kuondoa, isiondoe bashasha
Mana mkitizamia, utakuja wachemsha
Kumbe ndoa si ndoana, ni sehemu ya furaha

Tukisoma Qur'ani, tutakuwa wake wema
Mana hicho ndo kiini, kinachotwongoza vyema
Hututakuwa wahuni, bali ni waume wema
Kumbe ndoa si ndoana, ni sehemu ya furaha

Zuhura Iddi (**Mtunzi mtoto**)
Kitonga, Dar es salaam

AHMADIYYA UKOMBOZI DUNIANI

1. Kwa jina lako Jalia, Wa rehma na amani
Sisi umetujaalia, Masihi kumuamini
Hali hii kufikia, kwetu nyingi shukurani
Jamaat ya Ahmadiyya, ukombozi duniani

2. Limetufikia jua, sasa hatuko gizani
Twaitwa Waahmadiyya, kwenye yakini ya dini
Wenzetu walobakia, bado wana mtihani
Jamaat ya Ahmadiyya, ukombozi duniani

3. Shime tuoneshe njia, jitihada tufanyeni,
Mafunzo ya Jumuiya, kwa dhati tuyashikeni,
Kila kwenye familia, nidhamu hii jengeni
Jamaat ya Ahmadiyya, ukombozi duniani

4. Kwa kuwa twajivunia, hili ni kundi makini
Tuhubiri Jumuiya, bila ya hofu moyoni
Juhudi inatakiwa, kuimarisha imani
Jamaat ya Ahmadiyya, ukombozi duniani

5. Wapinzani wanalia, kila pembe duniani
Kuishinda Ahmadiyya, hilo haliwezekani
Kwao kilichobakia, kudumisha upinzani
Jamaat ya Ahmadiyya, ukombozi duniani

6. Allah Uliyetimia, Ituzidishie imani
Tuishike hii njia, yenye ukweli wa dini
Ingawa wanaumia, wote walio pembeni
Jamaat ya Ahmadiyya, ukombozi duniani

7. Hawa wanakusudia, kutaka kuvuruga dini
Ukweli ukitakiwa, wala haufichikani
Kila yanayotakiwa, wanayaweka pembeni
Jamaat ya Ahmadiyya, ukombozi duniani

8. Tabia zao za mila, wanachanganya na dini
Kubwa ya kwao dhamira, maslahi duniani
Wanafanya kila hila, kuivuruga imani
Jamaat ya Ahmadiyya, ukombozi duniani

9. Mkombozi kaingia, ndugu zetu waambieni
Wajiunge Ahmadiyya, kwenye Adili ya dini
Kama watapuuzia, mwisho wao mashakani
Jamaat ya Ahmadiyya, ukombozi duniani

10. waliopotea njia, na tuwakaribisheni
Hima wapate ingia, kabla kalantini
Wasije wakajutia, geti likipigwa pini
Jamaat ya Ahmadiyya, ukombozi duniani

11. Tuliyo Waahmadiyya, raha, furaha moyoni
Wa nje ya Ahmadiyya, aibu misikitini
Wanadili na Dunia, sio sana ya kidini
Jamaat ya Ahmadiyya, ukombozi duniani

12. Kalam naachia, kazi kwetu waumini
Tuhubiri jumuiya, tunusuru hii dini
Tutafute kila njia, za busara na amani
Jamaat ya Ahmadiyya, ukombozi duniani

Kassim Mohamed Mlekeni,
Ikwiriri, Rufiji, Pwani

KIENEZE KISWAHILI

Ya Rabi Mola Karima, Jinalo ndio awali
Awali kwa kulisema, naomba nitakabali
Pia nijaze hekima, niseme yanostahili
Kieneze Kiswahili, kienee duniani

Ni sisi tunaosema, lugha hii Kiswahili
Tuongeze wetu wema, kusema yanostahili
Na tuzidishe huruma, wageni wageni napowasili
Kieneze Kiswahili, kienee duniani

Hivyo karibuni sana, tujifunze Kiswahili
Ni lugha nzuri sana, kuongoza bara hili
Na dunia yote pana, kienee mpaka mbali
Kieneze Kiswahili, kienee duniani

Kwa kukuza urafiki, kwa watu kila mahali
Kutakifanya sitaki, kwa watu wa kila hali
Na tuiondoshe chuki, tung'arishe Kiswahili
Kieneze Kiswahili, kienee duniani

Tususahau Waarabu, kwa michango mbalimbali
Maneno ya Kiarabu, yang'aa kama miali
Ni mengi hasa ajabu, yalo kwenye Kiswahili
Kieneze Kiswahili, kienee duniani

Wakati tunatukuza, lugha hii Kiswahili
Ni lazima tukawaza, ni nini yake asili
Kutatupa mwangaza, kuweza kufika mbali
Kieneze Kiswahili, kienee duniani

Chini naweka kalamu, namuomba Ya Jalali
Uwajaze wanadamu, wafanye yalo adili
Ili wakuze elimu, uipendayo Jalali
Ili wakuze elimu, isiyo ya udhalali

Hassan Sango (**Jang-e-Mukaddas karatasini**)

RAZAKI

Yeye ndo mgawa riziki, Huruzuku kwa mafungu
Pindi tupatapo dhiki, Na kughubikwa machungu
Tusisahau huyu rafiki, Mtibu yote machungu
Nakushukuru razaki, Mtufaa kila hali

Watupa tustahilicho, So kila kile tombacho
Tugawapo bila choyo, Wongeza kipunguacho
Twaafiki unenayo, Na turadhi upendacho
Nakushuru razaki, Mtufaa kila hali

Shunda Mshundia Wana, Daluni, Tanga

Mapacha wa Fasihi

Kutoka uk.11

umoja wake ni vitu alivyoviweka maanani. Dhana yake juu ya uhuru ni kwamba binadamu amepewa heshima kubwa kuliko viumbe wengine. Ukitoa binadamu viumbe wengine vyote ni malaika. Vinatenda vile walivyoamrishwa. Binadamu pekee amepewa uhuru wa kuchagua '***Imma shaakiran wa imma kafura***'. Hivyo binadamu amezaliwa huru na lazima apambane kuikatilia mbali minyororo. Na katika shairi lake moja alisisitiza; ***Uhuru jambo halisi, na kuukosa ni taabu***.

Ili kupata shabaha ya uhuru, umoja ulitakiwa upatikane. Sauti moja na kiongozi madhubuti kusimamia harakati za uhuru. Sheikh Amri Abedi alisema Nyerere alikuwa na sifa za uongozi na hivyo akawaita watu wajiunge na TANU. Katika ubeti huo anasema;

Sauti ng'ambo ya nyota, ...
.....

Katika shairi hilo amesisitiza zaidi umoja, kwa sababu ni umoja ndio unaoleta ufaulu.

Shaabani Robert aliitumia kalamu kuonesha uonevu wa ukoloni na hivyo kutaka mabadiliko. Shairi lake la '*Rangi*' lilisisitiza usawa wa binadamu. Kwamba rangi haikuwa laana wala alama ya maafa. Binadamu sote tuko sawa na hakuna mwenye haki ya kumtawala mwingine. Ni wamoja walimwengu, walao mofa na dengu. Shaabani Robert aliwahimiza pia Waafrika wajiunge na TANU ili kupata uhuru.

KISWAHILI.

Washairi hawa wawili Shaabani Robert na sheikh Kaluta Amri Abedi walipenda na kuthamini lugha yetu adhimu Kiswahili. Walijiviringa na kujigaragaza katika kukienzi na kukitumia Kiswahili.

Shaabani Robert ameandnika riwaya na mashairi vyote hivyo vikiwa na dhamira ya kuendeleza Kiswahili. Alikuwa pia mjumbe wa kamati ya Kiswahili katika Afrika ya Mashariki. Mchango wake katika kamati hiyo ulienziwa sana na kuheshimiwa. Washairi walipoanzisha chama chao mwaka 1959 pale katika ukumbi wa Ahmadiyya –Masjid Salaam, Dar es salaam Shaabani Robert licha ya kutokuwepo katika mkutano huo alikuwa amempeleka mwanae shuleni Uganda alichaguliwa kuwa Karii pamoja na Sheikh Amri.

Sheikh Kaluta Amri Abedi alitumikia Kiswahili toka akiwa kijana wa miaka 13 alipoanza kutunga mashairi. Wakati alipojiunga na Jumuiyya ya Waislam wa Ahmadiyya mwaka 1937 alishiriki katika kutafsiri vitabu vya Jumuiyya ya Ahmadiyya. Mchango mkubwa hata hivyo ulikuwa katika kusaidia katika kutafsiri Kurani Tukufu kwa Kiswahili iliyotolewa na Ahmadiyya mwaka 1953.

Mwaka huo wa 1953 sheikh Amri alitoa kitabu cha '*Sheria za kutunga mashairi na diwani ya Amri*' ambacho kimeeneza elimu ya ushairi. Alipoteuliwa kuwa Waziri wa Sheria moja ya jukumu lake alilopewa na Mwalimu Julius K. Nyerere ni kusaidia na kusimamia harakati za kuweka sheria za nchi katika lugha ya Kiswahili. Kamati iliundwa ya kutafsiri sheria miongoni mwa wajumbe walikuwa ni Lydon Harris, Matias Mnyampala, Mohammed Ali na Mwalimu Feruzi Hemedi Mbaya. Kamati hii ilifanya kazi nzuri sana na baadhi ya sheria zilitafsiriwa katika Kiswahili.

Licha ya kuonesha kwa vitendo mapenzi yao katika lugha ya Kiswahili, wote walitunga shairi linaloonesha hisia kali na mapenzi ya dhati kwa lugha ya Kiswahili. Shaabani Robert anakumbukwa kwa shairi lake; '*Titi la mama ni tamu, jingine halishi hamu*'. Nae Sheikh Kaluta Amri Abedi alitoa hisia zake za ndani kuhusu Kiswahili katika sehemu mbili; alipokuwa na majonzi kuhusu kifo cha simba wa Uswahilini (Shaabani Robert) na alipomuonya Mwalimu wa vijijini ambaye sawa na Sheikh Amri bwana huyo alikuwa anatobanga Kiswahili. Katika ile majonzi ya kuombeleza kifo cha Shaabani Robert sheikh Amri anaomboleza;

Haya msiba mzito, amefishwa Shaabani
Nyoyo zinawaka moto, imetushika huzuni,
Lugha yetu bado toto, mlezi sasa ni nani?

Na kuhusu huyu aliyetobanga lugha anamuonya;

Ulugha kuvungavunga, hebu punguza sarange
Elimu ya kubananga, mwenyewe kalie nyange
Haturidhii ujinga, hatutwai lau tonge

Mapacha hawa wamefanya kazi nzuri na mcheza kwao hutunzwa. Na zawadi pekee tunayoweza kuwapa ni kukilinda na kukienzi Kiswahili.

TAFUTA MANENO

Tafuta maneno 24 hapo chini kwa kuyazungushia na Penseli

N	C	G	M	A	P	I	N	D	U	Z	I	M	K	L	M
T	L	N	L	B	G	L	B	W	S	G	L	R	J	N	A
S	P	M	I	B	U	G	H	U	D	H	A	L	D	L	H
H	Y	L	M	S	S	M	K	N	B	L	A	K	M	U	A
U	W	J	L	E	A	A	D	I	P	I	I	I	R	H	R
R	Z	L	P	N	J	B	L	G	S	H	L	A	R	K	I
A	Y	K	R	S	H	V	X	A	S	U	B	E	M	I	M
M	V	J	D	A	M	J	V	I	N	U	D	U	S	G	U
B	W	E	R	E	R	E	L	L	R	A	B	A	M	H	M
A	N	D	G	R	T	I	A	A	U	A	L	J	A	D	I
F	W	I	Y	R	K	O	B	K	L	A	M	A	U	K	G
R	F	F	D	A	K	R	U	A	G	D	L	N	D	K	N
I	L	F	R	A	M	B	H	N	G	F	B	N	H	F	D
T	J	A	R	F	H	G	U	K	R	L	D	A	M	N	T
I	T	A	Z	T	A	B	L	B	Z	B	U	R	A	H	I
Q	B	R	I	S	I	T	I	M	A	J	I	L	I	S	I

Tarakilishi	Shairi	Barubaru	Afriti
Bughudha	Maud	Bwerere	NIDA
Bileshi	Barakoa	Kisu	Buku
Sensa	Risiti	Janna	Majilisi
Aghalabu	Salana	Mapinduzi	Nisab
Burahi	Maharimu	Bungala	Shura

UNGANISHA NUKTA

Unganisha nukta ili upate picha moja iliyokamilika.



Jinsi ya kupika Chapati za viazi

Na **Mtandao**



MAHITAJI

DONGE

1. **Unga wa ngano vikombe 4**
2. **Mafuta viJiko 2 chakula**
3. **Maji kiasi**
4. **Siagi ½ kikombe**

UPANDE WA VIAZI

1. **Viazi vilivyochemshwa na kupondwa 4**
2. **Chumvi kiasi**
3. **Binzari ya unga ½ kiJiko chai**
4. **Pilipili ya unga ½ kiJiko chai/ukipenda**
5. **Kitunguu kilichokatwa katwa 1**

JINSI YA KUPIKA

1. Changanya mahitaji yote ya unga kisha kanda kufanya unga mlaini.

2. Funika acha ukae ½ saa, fanya madonge size upendayo.

3. Changanya mahitaji yote ya viazi weka pembeni.

4. Chukua donge moja sukuma kufanya chapati ndogo, chota mchanganyiko wa viazi kisha funika vizur na zungusha kufanya donge tena. Rudia kwa madonge yote.

5. Sukuma chapati zako na choma kama kawaida katika moto wa kiasi hadi zipate rang nzuri.

6. Chapati za viazi tayari kwa kula na *curry* yoyote.

NB; Ukiwa unashushia na fanta pembeni lazima usahau shida za dunia😋

KUTOKA MAKTABA

Na Ally Hamisi Mbambwa

Mahubiri katika nchi ya Hispania

Maulana Karam llahi Zafar Sahib.

Alipenda kuwaambia wateja wake kuwa, "***Uturi anaowauzia manukato yake hayadumu muda mrefu, bali yapo manukato yenye uturi unaodumu muda wote nayo ni mafundisho ya Islam***". Hatimaye aligundulika!.

Alipata mashambulizi kutoka kila upande. Nguvu za dola, mara nyingi walimkamata na kumtupa gerezani. Wafia dini wa miji ya Hispania, mara kadhaa walimfanyia fujo, kumpora na hata kuyamwaga manukato yake. Lakini misukosuko yote hiyo ilimuimarisha badala ya kumkatisha tamaa.

Alifanikiwa kutafsiri vitabu viwili kwa lugha ya Spanish moja ya kitabu ni *Hekima ya Mafundisho ya Islam* na alimpelekea zawadi mtawala wa wakati huo Dikteta Fransisco Franco.

Maulana Karam llahi Zafar Aahib, mwaka 1969 akamuandikia barua mtawala huyo akimueleza ukweli wa mafundisho ya Islam kuwa, Mwenyezi Mungu ni mmoja, akaeleza cheo na daraja la Mtume Muhammad^{saw}, Safari ya Hadhrat Isa^{as} baada ya tukio la msalaba na madai ya Hadhrat Ahmad^{as}.

Tarehe 24 Desemba, Katibu wa Dikteta Fransisco Franco alimletea barua ya shukrani kutoka kwa mtawala.

Maulana Karam llahi zafar sahib aliihifadhi barua ile vizuri kwenye frem ya kioo na hapo akanza kuhubiri waziwazi. Na pindi alipokamatwa na askari, alionesha barua ile ya pongezi kutoka kwa Rais wa nchi iliyokuwa na saini na muhuri wa ikulu, askari wakagwaya!.

Kutokana na vuguvugu la mahubiri na barua aliyompelekea Rais wa nchi, mwaka 1971 serikali ilitoa uhuri wa kuabudu kwa dini zingine na jumuiya ikasajiliwa rasmi.

Chini ya usimamizi wa Khalifatul Masih III Hadhrat Mirza Nasir Ahmad^{rh}, Tarehe 9 Oktoba, 1980 Aliweka jiwe la msingi la msikiti katika mji wa pedro Abadi ***Masjid Basharat*** ambao ndio **msikiti wa kwanza** kujengwa katika Hispania baada ya miaka 500 tangu dola ya kiislam kuanguka.

Ni katika sherehe za kuweka jiwe la msingi la msikiti huo, ndio siku **kauli mbiu** maarufu ya jamaat Ahmadiyya iliasisiwa na Khalifa Mtukufu wa tatu, Hadhrat Mirza Nasir Ahmad^{rh} ya **Love for All Hatred for None**..... Mashallah!

Masjid Basharat, ulifunguliwa na Khalifa Mtukufu wa nne, Hadhrat Mirza Tahir Ahmad^{rh} Tarehe 10 Septemba 1982.

Tunamuomba **Allah**^{swt} Ampe Malipo mema kwa Juhudi kubwa aliyoifanya **Maulana Karam llahi Zafar Sahib**. Allahumma Amin.

Nyongeza:

Khalifa Mtukufu wa tano Hadhrat Mirza Masroor Ahmad^{atba}, Tarehe 29 March, 2013 alifungua *msikiti wa pili* katika mji wa Valencia Hispania unaoitwa **Baitur Rahman** . Alhmadulillah thumma Alhamdulillah.

****

Itaendelea Inshallah

ASEMAVYO MASIHI ALIYEAHIDIWA^{as}

Enyi msiofahamu, fahamuni vizuri, Enyi mlioghafilika, zingatieni barabara kuwa hamwezi kuachiliwa pasipo utakaso wa kweli wa kiimani, kikhulka na kiamali. Na yule akibaki mchafu kwa kila jiha, kisha anajifahamu kuwa yu mwislamu, yeye hamdanganyi Mwanyezi Mungu, bali anajidanganya mwenyewe. Nahusianaje na wale wasiojitwika amri za dini kwa moyo wa kweli wala hawashikamani na ukweli, wala hawapendi kuzichukia njia za kifasiki, wala hawatengani na vikao zinamofanywa dhihaka, wala hawaachani na mawazo machafu, wala hawashikamani na utu, ustaarabu, Subira na upole; bali wanawasumbua wenye hali ndogo na kuwafukuza wanyonge, wanatembea masokoni kwa maringo, wanajikalia vitini kwa kiburi na wanajifahamu wao ndio wakubwa, lakini hakuna mkubwa ila yule ajifahamuye yu mdogo. Wamebarikiwa wale wanaojiona hakiri na wadogo na wanazungumza kwa hay ana wanaheshimu wenye hali ndogo na masikini na kuwastahi wanyonge, hawadhihaki kwa ujeuri na majivuno,na wanamkumbuka Mola wao mkarimu na hutembea juu ya ardhi kwa unyenyekevu.

Basi, nakariri kusema kuwa hao ndio watu waliotayarishiwa Pepo. Na yule ambaye duniani humu hayuko nje ya jahanamu na jeuri, kiburi, majisifu, majivuno, anasa za dunia, uchoyo na maovu, katu hatakuwa nje yake huko Akhera pia. Nifanyaje, na kutoka wapi nilete yale maneno zitakayoziathiri nyoyo za kikundi hilo. Ee Mungu, nijalie yale maneno na nifunulie zile hotuba ambazo zitilie mioyo yao nuru yake na kuiondolea mbali sumu yao kwa athari ya sifa yake ya kiua sumu. Roho yangu inasumbuka kwa shauku ya kuwa iwadie ile siku ambapo niwaone katika jumuiya yangu, watu wengi waliokwisha achana na uwongo kikweli na kufunga ahadi ya kweli na Mungu wao kwamba wataepukana na kila shari na kutengana kabisa na kiburi kilicho asili ya jeuri zote, na watadumu kumcha Mola wao. Lakin hadi sasa sioni sura kama hizi isipokuwa watu waache mahususi. Naam, wanasali wasijue sala ni kitu gani. Mpaka moyo ufanye sijida ya unyenyekevu, kuzitegemea sijida za dhahiri na tamaa ya bure. Kama damu ya nyama za dhabihu zisivyomfikia Mungu, bali utawa pekee unamfikia, ndivyo hivyo rukuu na sijida za kimwili zilivyo bure maadamu rukuu na sijida za moyo hakuna. Moyo kusimamia katika ibada ni kutekeleza amri za Mungu, rukuu ni kuelekea kwake na sijida ndiyo kutengana na nafsi yake. Basi, ni masikitiko, masikitiko elfu, ya kwamba sioni ndani yao athari yoyote ya maneno haya, lakini naomba dua, na nitadumu kuomba maadamu nipo hai, na dua yeneyewe ndiyo hii hii kuwa Mwenyezi Mungu azitakase nyoyo za jumuiya yangu hii, na kwa kurefusha mkono wa rehema yake Azielekeze nyoyo zao kwake na kuziondolea mbali nyoyoni mwao jeuri zote na inda na kuwajalia wapendane kikweli. Ninayo yakini dua yangu hii wakati fulani itapokelewa na Mungu Hatapoteza bure dua zangu. Naam, naomba pia kuwa kama yupo ndani ya Jumuiya yangu mtu aliye mwenye bahati mbaya kwa kudumu katika elimu na nia ya Mungu, ambaye hana bahati ya kujipatia utakaso wa kweli na hofu ya Mungu, basi, Ee Mungu, Umgeuze kwangu aende upande mwingine jinsi alivyogeuka kwako, na badala yake umlete mwingine aliye mpole wa moyo ambaye roho yake inakutafuta wewe. Hali yangu sasa ni kuwa namwogopa mwenye kufanya baiati jinsi mtu amwogopavyo simba, kwani sitaki mtu akiwa kidudu cha dunia aungane nami." (Ushahidi wa Kuran uk.219-222 chapa ya 2018)

MATUKIO KATIKA PICHA



Amir Jamaat akitoa zawadi kwa Afisa Elimu Mkoa wa Geita aliyemuwakilisha Mkuu wa Mkoa





Ufungaji Jalsa Salana Geita kwa Maombi yaliyoongozwa na Amir na Mbashiri Mkuu



Gari ya Polisi ikiongoza msafara wa Amir Jamaat alipokuwa akielekea katika Jalsa Salana Shinyanga



Amir na Mbashiri Mkuu akitoa zawadi za kielimu kwa wanajamaat katika Jalsa Salana Simiyu



Amir Jamaat akizungumza na Mkuu wa Wilaya ya Itilima Mh. Feiza Salehe katika Jalsa Salana Simiyu



Picha ya pamoja baada ya ufunguzi wa nyumba ya Mwalimu Mwamala, Shinyanga



Ufunguzi wa msikiti na kisima cha Maji Igunda, Shinyanga ulioongozwa na Amir na Mbashiri Mkuu



Picha ya pamoja baada ya ufunguzi wa msikiti, na Kisima Kalo, Shinyanga



Picha ya pamoja baada ya ufunguzi wa msikiti, nyumba ya Mwalimu na Kisima Luhuha, Geita



Amir Jamaat akihutubia wahudhuriaji wa ufunguzi wa Nyumba ya Mwalimu Nhumbili, Shinyanga

Kiswahili - Toka jana hadi leo

Kutoka uk. 5

kutoka kwa watu wa zama zake wala katika taarifa za kihistoria za ufalmew wa zama hizo ambazo inasemekana uliwategemea watu kama Muyaka kwa ushauri wa maamuzi juu ya mambo mbalimbali.

Inakisiwa tu kwamba bwana Mwengo aliishi katika miaka ya 1700 na aliishi Pate, na inasimuliwa kuwa Sultan wa Pate alimtaka aandike kitabu ambacho kingetokea kuwa moja ya misahafu ya fasihi ya Kiswahili. La! Haula, maktaba ya Sultani wa Pate iliteketea pamoja na kasri lake mwanzoni mwa karne ya 19.

Nyaraka chache za kipindi hicho cha mwanzo huenda ziliokolewa kwa kutwaliwa na familia binafsi, ambazo watu wake walizitunza kama urithi wa ukoo, na hata baada ya maanguko ya koo za Kiswahili watu hao walikuwa wagumu kuzitoa nyaraka hizo, kuziazimisha na hata kuzionyesha johari zao hizo kwa watu wa nje. Walizihifadhi katika viriba vya ngozi, shaba na hata dhahabu na fedha, walijivunia kuwa ni mirathi ya kihistoria kutoka wahenga wao. Hili pia liliongeza usiri mkubwa juu ya historia ya Kiswahili na waswahili wenyewe. Ndiyo maana tunaona kwamba uhaba wa maandishi juu ya historia ya Kiswahili na waandishi wake umeendelea kubaki katika kiza kinene.

Tofauti na ilivyo kwa Waingereza kwa mfano; William Shakespeare, Bernard Shaw, n.k. ni miongoni mwa washairi wa mwisho maarufu wa lugha hiyo. Vitabu vilivyoandikwa juu ya kila mmoja wao vinazidi mara nyingi idadi ya vitabu vyote vilivyopo kuwahusu waandishi wote wa Kiswahili. Cha ajabu ni kwamba hata hivyo vichache vilivyopo, kuhus waswahili, vingi vyao vimeandikwa na watu wa nje, kama vile Wajerumani na Waingereza waliotamalaki katika – Biladi Swahiliya – miji ya waswahili kuanzia mwishoni mwa karne ya 19.

Katika kuandika kwao waaandishi hao wa kigeni walitegemea mno simulizi kutoka kwa baadhi ya ulamaa wa Kiswahili waliokuwako nyakati hizo. Washairi kama Maalim Yahya Ali alitumainiwa zaidi kkwa habari za Muyaka na Bwana Mataka wa Siu kwa kuwa inasemekana alisoma mno maelezo yao katika vyuo vya pale Yunga, Lamu na Mombasa.

Kwa hali hii inajidhihirisha kuwa waandishi wa kigeni nao walichangia kiasi chao katika kujenga uwepo wa Kiswahili. Kwa maana katika zama zile za wakoloni wa Kijerumani Kiswahili kilitambuliwa miongoni mwa lugha rasmi. Wakati huo moja ya kigezo cha mtu kupewa uliwali ilikuwa ni ujuzi wa kusoma na kuandika Kiswahili. Bado wakati huo kiliandikwa kwa herufi za Kiarabu na taratibu kutoka hapo herufi za sasa za Kilatini zikachukua nafasi.

Asili ya Kiswahili

Na **Mwl Abdullah Mbanga**
Redio AHmadiyya, Mtwara

Kiswahili ni kito cha thamani ambacho yumkini kimekosa bahati ya kutunzwa. Kiswahili ni lugha ambayo kama ingepembejewa kwa jino na ukucha, bila shaka ingefanikiwa kuunganisha juhudi za watu wa bara zima la Afrika katika shabaha moja. Kwa maana ni lugha hii tu, iliyo lugha ya Taifa ya nchi yetu, ndiyo mabayo hakuna kabila linaloweza kujinadi kuwa ni lugha yake ya asili.

Kiswahili ni lugha yenye sura ya utaifa sio kwa Tanzania tu, bali ni mkusanyiko wa lahaja nyingi za Wabantu, inakusanya lahaja zaidi ya elfu za kibantu ambazo zilitandawaa sehemu kubwa ya Afrika iilyo kusini mwa Ikweta, zikafika hadi kaskazini yake katika maeneo ya Cameroon, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, bila kusahau Uganda na pia Kenya nchi ambayo inaaminiwa kuwa ndiko eneo ambapo Kiswahili kilizaliwa. Kuna ushahidi kwamba Kiswahili halisi pia kilikuwa lugha rasmi katika maeneo ya Somalia, kwa maana hata katika Mogadishu kuna eneo liitwalo Shangani (yaani mchangani). Hii inaonyesha pia nchi hii ilikuwa ni himaya ya Waswahili kabla hawajatimuliwa na wahamiaji wa Kisomali katika karne ya 16 na baadaye. Ndiyo maana tukaona hata sasa katika miji kama Barawa na Kismayu (jina limaanishalo kisima cha juu) Kiswahili ndiyo lugha rasmi hata sasa. Na watu wa huko hawana kabila nao hawajitambulishi kama Wasomali bali hujiita Wabarawa au Waswahili. Hali kadhalika kuna visiwa vilivyo katika pwani ya Somalia vinavyoitwa magunyani ambako pia ni kituo kikuu cha Kiswahili.

Upande wa kusini wa himaya ya Kiswahili hufikia hadi kaskazini mwa Msumbiji. Na inasemwa hata jina lenyewe la nchi msumbiji asili yake ni Kiswahili. Hivyo yote iliyo baina ya Somalia na Msumbiji tangu zama za hati ilijulikana kama – The Swahili Coast – na wasomi wa Kiarabu ambao ndio waliokuwa taifa kubwa wakati huo waliita miji hiyo kuwa Bilaadus – sawahili yaani miji ya watu wa pwani.

Hadi leo, visiwa vyote vilivyopo katika ukanda huu kama Comoro, Mauritius na Shelisheli bado ni za waswahili. Kiswahili kama lugha ya biashara ilizungumzwa pia katika pwani ya Aden. Ilifika mbali hadi Suez na ikateremka kusini hadi majunga kaskazini mwa Madagascar.

Kikiwa lugha kuu ya biashara, Kiswahili kilipelekwa bara na wachuuzi waliokwenda kubadilishana nguo za kitani za India kwa vipusa. Safari ya uchuuzi ya kusini ilianzia Kilwa kusini-mashariki hadi kusini mwa ziwa Nyasa. Msafara wa kati ulianzia Bagamoyo, kupitia tabora (yaani kambini - kwa Kiswahili) hadi Ujiji (mjini - kwa kiswahili) katika ziwa Tanganyika, kutoka hapo ulielekea Kasongo katika mto Lualaba na baadaye kuelekea kaskazini katika mji wa Kisangani ambao kwa jina lake hilo inaaminika ulianzishwa na waswahili (kisangani – humaanisha – kichangani). Msafara wa ksakazini ulianzia Mombasa kuelekea magharibi hadi Mwanza katika ziwa Nyanza hadi pale eneo hilo lilipokosa amani baada ya kuvamiwa na Wamasai katika karne ya 19. Pia kulikuwa na misafara mifupi mifupi iliyotoka Kilifi hadi mto Voi, malindi kuelekea Sabahi, au Galana na kutoka Kipimo kupitia Garisemo hadi mto Tana, msafara huu ilifika hadi sehemu ya katikati ambapo inaamimika ndipo palipowahi kuwa na Dola ya mfalme Kaffa inaayotajwa na mwandishi H. Ridder Haggard katika kitabu cha Mashimo ya Mfalme Suleiman kama ni nchi ya Wakukuana. Inawezekana pia jina la mfalme huyu ilikuwa ni lakabu aliyopewa na Waarabu, waliokuwa wachuuzi wakuu enzi hizo neno Kaffa humaanisha "atoshaye au afaaye'.

Kwa mujibu wa utamaduni wao, waswahili walijiita waungwana au walungwana.

Inasimuliwa kuwa, mtalii msomi wa Kiarabu Al-mas'ud alifika Mombasa kunako karne ya kumi (BK) na akanukuu maneno machache ya lugha ya hapo ambayo yeye aliita kizinji. Maneno ambayo Al-Mas'ud aliyaandika mabayo yanapatikana katika nyaraka za kale ni MUKULU IJUKU, ni maneno mawili ya Kiswahili yamaanishayo Mkuu Juu. Neno la tatu ambalo alilinukuu ni Kilazi ambalo kwa Kiswahili cha sasa hutamkwa kiazi.

Hii inatuonyesha kwamba Kiswahili kilikuwa kikizungumzwa tangu enzi hizo – karne ya kumi BK – ingawa kadiri lugha inavyoendelea baadhi ya matamshi hubadilika kulingana na hali ya watamkaji na wakati lakini kwa vyovyote muundo wake ulibaki katika asili yake.

Miongozo muhimu kwa wasomaji wa Quran Tukufu na wasikilizaji

Na Sheikh Mussa ibn Issa
Mtwara

9. Suratul-Mulku Aya ya 31; Msomaji au msikilizaji asomapo au kusikiliza maneno فَمَنْ يَأْتِيكُمْ بِمَاءٍ مَعِينٍ Kwamba*; Basi nani atakuleteeni maji safi yatiririkayo?* anakiwa kuitikia kwa kutamka maneno haya اللهُ يَأْتِينَا بِهِ وَهُوَ رَبُّ الْعَالَمِيْنَ kwamba; *Allah atatuletea kwani yeye ndio Mola wa walimwengu.*

10. Katika suratul-Baqarah aya ya 200 isemayo;

ثُمَّ أَفِيضُوا مِنْ حَيْثُ أَفَاضَ النَّاسُ وَاسْتَغْفِرُوا اللَّ إِنَّ اللَّ غَفُورٌ رَحِيمٌ

Kisha miminikeni toka mahali wamiminikapo watu,na ombeni msamaha kwa Allah, hakika Allah ni Msamehevu Mrehemevu.

Na Suratul-Nnisaa ayah ya 107 isemayo: وَاسْتَغْفِرِ اللَّ إِنَّ اللَّ كَانَ غَفُورًا رَحِيمًا

Na omba msamaha kwa Allah, kwa hakika Allah ni Msamehevu mrehemevu.

Msomaji au msikilizaji asomapo au kusikiliza Aya hizi anapaswa kuitikia kwa kutamka maneno haya; أَسْتَغْفِرُ اللهَ *Namuomba msamaha Allah.*

11. Msomaji au msikilizaji wa Quran Tukufu asomapo au kusikiliza Sural-Ghashiyah Aya 26-27 zisemazo; إِنَّ إِلَيْنَا إِيَابَهُمْ ○ ثُمَّ إِنَّ عَلَيْنَا حِسَابَهُ م○

Hakika marejeo yao ni kwetu ; Bila shaka hesabu yao ni kwetu.

Basi itampasa kuitikia kwa kutamka maneno mwishoni;

اللهُمَّ حَاسِبْنَا حِسَابًا يَسِيْرً ا *Ee Allah tuhesabie hesabu nyepesi.*

12. Aya ya Mwisho ya suratu tiin aya 9 isemayo; أَلَيْسَ اللَّ بِأَحْكَمِ الْحَاكِمِينَ

Tafsiri yake; *Je, Allah si hakimu bora kuliko Mahakimu?*

Msomaji au msikilizaji asomapo au kusikiliza Aya hii itampasa kuitikia kwa kutamka maneno haya; بَلَي وَنَحْنُ عَلَي ذَالِكَ مِنَ الشَّاهِدِيْنَ *Naam, na sisi tu miongoni mwa mashahidi.*

13. Suratu Nasri aya 4 isemayo; فَسَب حْ بِحَمْدِ رَب كَ وَاسْتَغْفِرْ ه yaani; *Basi Mtukuze Mola wako kwa sifa njema,na umuombe msamaha.*

Msomaji au msikilizaji asomapo au kusikiliza Aya hii itampasa kuitikia kwa kutamka maneno yafuatayo; سُبْحَانَكَ اللهُمَّ رَبَّنَا وَ بِحَمْدِكَ اللهُمَّ اغْفِرْلِ

Utakaso ni wako Ee Allah, sifa zote njema ni zako Ee Mola wetu, nisamehe.

14. Suratul-Waqiyah kuanzia Aya 60 hadi 73 zisemazo;

أَأَنْتُمْ تَخْلُقُونَهُ أَمْ نَحْنُ الْخَالِقُونَ *je mmeiumba ninyi au tumeiumba sisi?*

Msomaji au msikilizaji ataitikia kwa kutamka maneno haya; بَلْ أَنْتَ يَا رَ بِ

kwamba; *Bali ni wewe Mola wangu.*

Vile vile katika Aya 65 isemayo; أَأَنْتُمْ تَزْرَعُونَهُ أَمْ نَحْنُ الزَّارِعُونَ kwamba; *Je, ni ninyi mmeiotesha au tumeiotesha sisi?* Ataikia kwa kusema بَلْ أَنْتَ يَا رَ بِ.

Vile vile katika Aya 70 isemayo; أَأَنْتُمْ أَنْزَلْتُمُوهُ مِنَ الْمُزْنِ أَمْ نَحْنُ الْمُنْزِلُونَ kwamba; J*e, ni ninyi mmeyateremsha kutoka mawinguni au ni sisi tuteremshao?* Ataitikia kwa kusema; بَلْ أَنْتَ يَا رَ بِ. kwamba; *Bali ni wewe Mola wangu.*

Vile vile Aya ya 73 isemayo; أَأَنْتُمْ أَنْشَأْتُمْ شَجَرَتَهَا أَمْ نَحْنُ الْمُنْشِئُونَ *Je,mti wake mmeuumba ninyi au sisi ndio tuumbao?* Ataitikia kwa kusema; بَلْ أَنْتَ يَا رَ بِ.

15. Suratu Yaasiin Aya 79 isemayo; قَالَ مَنْ يُحْيِي الْعِظَامَ وَهِيَ رَمِيمٌ *Akasema, nani atakayeihuisha mifupa haliyakuwa imesagika?*

Msomaji au msikilizaji atatakiwa kuitikia kwa kutamka maneno haya;

يُحْيِيْهَا الَّذِىْ اَنْشَاَهَا اَوَّلَ مَرَّةٍ وَّ هُوَ بِكُلِّ خَلْقٍ عَلِيْم

Ataihuisha aliyeiumba mara ya kwanza,naye ni mjuzi wa kila namna ya kuumba.

Vile vile Suratu YaaSiin Aya ya 82 isemayo;

أَوَلَيْسَ الَّذِي خَلَقَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ بِقَادِرٍ عَلَىٰ أَنْ يَخْلُقَ مِثْلَهُ م

Je, Aliyeziumba mbingu na ardhi hana uwezo wa kuumba mfano wao?

Ataitikia kwa kutamka maneno haya; بَلَىٰ وَهُوَ الْخَلَّقُ الْعَلِيمُ , *Naam, naye ni muumbaji mkuu, mjuzi.*

16. Suratu Shamsi Ayah 9 isemayo; فَأَلْهَمَهَا فُجُورَهَا وَتَقْوَاهَا *kisha akaifunulia maovu yake na wema wake.*

Msomaji au msikilizaji ataitikia kwa kutamka maneno haya;

اللهُمَّ آتِ نَفْسِيْ تَقْوَاهَا وَزَ كِهَا أَنْتَ خَيْرُ مَنْ زَكَّاهَا أَنْتَ وَلِيُّهَا وَمَوْلَهَ ا

Ee Allah ipe nafsi yangu taqwa (ucha Mungu) na uitakase kwani Wewe ndio Mbora wa waitakasao na Wewe Ndiye walii wake na Mlinzi wake.

17. Suratul-Ahzaab Aya 57 isemayo;

إِنَّ اللَّ وَمَلَئِكَتَهُ يُصَلُّونَ عَلَى النَّبِ ي يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا صَلُّوا عَلَيْهِ وَسَلِ مُوا تَسْلِيمً ا

Hakika Allah na Malaika wake humsalia Mtume; enyi waminio,msalieni (Mtume saw) na muombeeni amani.

Msomaji au msikilizaji asomapo au kusikiliza Aya hii anatakiwa kuitikia kwa kutamka maneno yafuatayo;

السَّلَمُ عَلَيْكَ أَيُّهَا النَّ بِيُّ وَرَحْمَةُ اللهِ وَبَرَكَاتُه اللهُمَّ صَ ل عَلَي مُحَمَّدٍ

Mapacha wa Fasihi

Kutoka uk.12

Tukishauvua mwili huu tutapata mwili mwingine na kuendelea. Shaabani Robert ana huzuni iliyochanganyika na matumaini;

Amina umejitenga, kufa umetangulia
Kama ua umefunga, baada ya kuchanua,
Nakuombea mwanga, peponi kukubaliwa,
Mapenzi tuliyofunga, hapana wa kufungua.

Nasadiki haziozi, roho hazitapotea
Twafuata uokozi, kwa mauti kutujia.

Ilimchukua Shaabani Robert miaka mingi kabla hajapata jiko jingine.

Sheikh Kaluta Amri Abedi alioa mapema bado yupo shuleni. Mke wake wa kwanza aliitwa Zamda binti Sudi, baadae alimpa jina la Shani. Ulitokea mgogoro mkubwa kutokana na mambo ya dini. Mgogoro huu umejitokeza vizuri katika '*Diwani ya Sheikh Kaluta Amri Abedi*', wakati anaandikiana na mpwawe Saadani Abdul Kandoro. Ni katika ndoa hii ndipo alipopata mtoto wake wa kwanza Bi. Radhia. Mwaka 1948 alioa mke wa pili Aziza Rajabu. Mke wa tatu ni Bi. Amina Mlezi ambaye alizaa nae watoto wafuatao; Bakri, Ummi, Sukheiri, Amiri, Adili na Shafii.

Washairi hawa walikuwa na mapenzi makubwa kwa watoto wao. Shaabani Robert aliwatungia tenzi kwa vijana wake wa kiume ili kuwapa mawaidha. Huu ni mtindo wa toka zamani miongoni mwa Washairi kuwapa mawaidha watoto wao. Kwa mfano utenzi maarufu wa '*Mwana Kupona*'.

Shaabani Robert kwa binti yake anamwambia;

Leo nataka binti,
Ukae juu ya kiti,
Ili niandike hati,
Hati ndogo ya wasia.

Na kwa mvulana alisema;

Kijana leta kalamu,
Nina habari muhimu,
Napenda uifahamu,
Dadayo kisha zamuye.

Ni tenzi zenye kuwafunza adabu njema na utii. Ni tenzi zilizojaa falsafa kuhusu namna ya kupita katika msitu huu wa maisha ambao umezungukwa na miiba kulia na kushoto. Na Shaabani Robert anasisitiza;

Kukinai jifundishe,
Kidogo kwako kitoshe,
Kikubwa sijizoeshe,
Kukijua kwa hatua.

Pato lako la halali,
Japo ni kitu dhalili,
Ni bora kuliko mali,
Fedheha inayotia.

Sheikh Kaluta Amri Abedi kwa muda mrefu, alikuwa na binti mmoja Bi. Radhia. Kutokana na ule mgogoro wa dini ilibidi atengane na mke wake. Kuondoka kwa mama Radhia kulileta huzuni nyumbani kwa Sheikh Amri na Radhia alikuwa mpweke. Kuziba pengo hilo alimtungia binti yake shairi ambalo lina mguso mkali. Na bi. Radhia kila alipolisoma shairi hilo machozi yalikuwa yanamdondoka.

Mama yangu simuoni, naambiwa kakimbia
Sina furaha moyoni, mama nilimzoea
Nimebaki ukiwani, ninalia na dunia.
Kinda ningali mtini, sina mama kunilea

Kwa mke wa tatu bi. Amina Mlezi Sheikh Kaluta Amri Abedi alipata watoto saba aliowalea kwa mapenzi makubwa licha ya kuwa na muda kidogo kutokana na shguhuli za kiserikali. Lakini kila alipopata nafasi alizungumza nao na kuwapigia hadithi za kuwaburudisha. Alichopenda zaidi ni kuwaeleza mambo ya dini. Siku moja aliwapa vitabu vya dini na kwa sababu walikuwa katika shule ya Agha Khan ambako walikuwa wanajifunza kwa Kiingereza, asubuhi yake alikwenda kuwatoa akina Abedi, Ummi na Sukheri na kuwapeleka shule za uswahilini. Tukio hilo pia analieleza rafiki yake mkubwa Matias Mnyampala. Kilichomuudhi aliwapata vitabu vya Kiswahili kusoma na wakashindwa na hivyo akaona ya kwamba hiyo haifai hata kidogo. Ukitizama kwa makini wazungupule hawa waliheshimu dini na walichosisitiza ni kusema na kutenda. Na kama anavyosisitiza Shaabani Robert katika *'Adili na nduguze'*; "*Tendo hukidhi haja, maridhawa kuliko neno*".

UHURU

Mapacha hawa wawili walikuwa na hasira kubwa kuhusu kutawaliwa. Walichukia hali hii na kwa kutumia kalamu wakaieleza jamii kwama binadamu alizaliwa huru, ni tabia ya ulafi wa binadamu iliyofanya binadamu waweze kuwanyonya na kuwadhulumu wengine. Na hatimaye kuwaweka kwenye minyororo isiyokwisha. Sheikh Kaluta Amri Abedi alichukua hatua za kuunda chama cha mafundi cherehani ili kupambana na unyonyaji. Alikuwa pia katika Tanganyika African Association na hiki ndio chama ambacho kilizaa TANU.

Kwa kupitia gazeti la *Mapenzi ya Mungu* alieleza jinsi Waafrika wangeliweza kutoka katika unyonge. Ukombozi wa Afrika na

Kifo Juu ya msalaba? Hoja kumi kutoka kwenye Biblia Takatifu

Kutoka toleo lililopita

10. MAOMBI YAKE YALIKUBALIWA

Kusoma kwetu Biblia kunadhihirisha kuwa Mungu huyasikiliza maombi ya Mitume wake na kuwaokoa na mateso na mitihani. Katika Agano Jipya tunasoma:

Yesu akainua macho yake juu akasema, Baba nakushukuru kwa kuwa umenisikia nami nalijua ya kuwa wewe wanisikia siku zote, lakini kwa ajili ya mkutano huu wanaohudhuria nalisema haya ili wapate kusadiki kwamba ndiwe uliyenituma. (Yohana 11:41-42). Tena tunasoma: *Akasema, Aba, Baba, yote yawezekana kwako, uniondole kikombe hiki, walakini si kama nitakavyo mimi, bali utakavyo wewe.* (Marko 14:36).

Sawa na nukuu hizo hapo juu ni Dhahiri Yesu aliogopa sana kuwekwa msalabani, hivyo aliomba kwa moyo mmoja aondolewe kikombe hicho kichungu. Yesu aliomba kwa unyenyekevu wa hali ya juu ili aondolewa aibu ya kufa kifo cha laana cha msalabani, angediriki vipi basi kwamba alikuwa ameishinda dunia kama angefia msalabani, kazi yake yote ingeharibika na wale wenye dhambi wangedadisi juu ya ukweli wa madai yake ya kuwa Nabii. Fikra ya yeye kufa msalabani haikubaliki. Akiwa Nabii wa Mwenyezi Mungu hakuogopa kifo hiki chakawaida, alichoogopa ni kifo cha msalabani kwani kifo cha namana hii kingeweza kueleweka kuwa ni kifo cha laana jambo ambalo lingekuwa kinyume na ujumbe wake wa kitume.

Siku hizi za mwili wake alimtolea yule, awezaye kumwokoa na kumtoa katika mauti, maombi na dua pamoja na kulia sana na machozi akasikilizwa kwa jinsi alivyokuwa mcha Mungu (5:7).

Hivyo inatubidi tuamini kwamba maombi hayo ya unyenyekevu wa hali ya juu bila shaka yalipokelewa na kimiujiza akaepukana na kifo cha msalabani na akaishi muda wa kutosha wa kuweza kufikisha ujumbe wake kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli huko mashariki: Akawaambia, *imenipasa kuihubiri Habari njema ya ufalme wa Mungu katika Miji mingine pia, maana kwa sababu hiyo nalitumwa.*

Ndugu wapendwa. Hoja hizi zinadhihirisha kwa fikra hizi za kusulubiwa kwa Kristo hazina ushahidi kutoka kwenye Biblia yenyewe. Hivyo ni wazi kuwa imani ya Kikristo iliyojengwa kwenye msingi huo mbovu haiwezi kuwa imara.

ENYI WAPENZI

Hoja hizi zinathibitisha kuwa wazo la kifo cha Yesu kwa kusulubiwa halithibitiki hata kutokana na mtazamo wa Biblia. Kwa hiyo, ni dhahiri kwamba imani ya sasa ya Ki-kristo msingi wake hauko sahihi wala hauna maana.



Picha ya Kaburi la Bwana Yesu Kristo (amani ya Mungu iwe juu yake) lililopo Mohallah Khanyar SRINAGAR, KASHMIR, INDIA jinsi linavyoonekana kwa nje na ndani. Picha na Bwana Mohammad Saeed Lone wa London

The First Muslim Newspaper in Swahili Language since 1936

MapenziyaMungu

DH. HIJ - MUHAR. 1444 AH | AGOSTI 2022 | ZAHOOR 1401 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufusaw

Abu Huraira*ra* anasimulia kwamba: Nilimsikia Mtume*saw* akisema: Abu Huraira wallahi mimi naomba msamaha kwa Allah kutubia kwake kwa siku moja zaidi ya mara sabini (**Bukhari**).

Mapacha wa Fasihi - Sheikh Shaabani Robert na Sheikh Amri Abedi Kaluta

Na **Mahmood Hamsini Mubiru**

Katika ulimwengu wa fasihi ya Kiswahili, Shaabani Robert na Sheikh Kaluta Amri Abedi wameamba kiajabu mithili kicha na kofia, sahani na kawa au chanda na pete. Mapacha hawa wawili wa fasihi waliheshimiana, walibadilishana mawazo na wakategemeana. Shaabani Robert anatoa ushahidi kwa hilo:-

Tukipangana wawili, kaskazi hata kusi
Zije kwa dhoruba kali, za kutufuata sisi
Twaweza kuzikabili, pasi na wasiwasi

Ukichunguza maandishi yao kwa makini, wanakubaliana katika mambo mengi licha ya kwamba walikuwa wanatofautiana kwa umri.

Shaabani Robert alizaliwa kandokando ya bahari ya hindi mwaka 1909 katika kijiji cha Vibambani Tanga ndio maana moja ya jina baba yake ni Ufukwe. Sheikh Kaluta Amri Abedi alizaliwa kama anavyoimba mwenyewe;

Kando ya mto wa maji,
Tanganyika kuna mji,
Unaoitwa Ujiji,
Nilizaliwa ghulamu.

Mwaka 1924.

Waandishi hawa wawili wameathiriwa kwa njia moja au nyingine na Islam. Ujiji ulikuwa mji maarufu wa biashara na kilikuwa kituo cha Waarabu wakiwa njiani kuelekea Kongo ambayo kwa hivi sasa inaitwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo. Athari za mafundisho ya Islam zinajitokeza bayana katika kazi za wazungupule hawa wawili. Wakati Sheikh Kaluta Amri Abedi anaanza kila jambo lake kwa Bismillahi – maana yake *naanza kwa jina la Allah*, Shaabani Robert anamshukuru Allah wakati alipostaafu na akimba;

Alhamdulillah - shukurani zote kwa Allah,
Namshukuru ilahi, Mwenyezi Mkamilifu,
Kwa kuishi nikawahi, kazini kustaafu,
Bado ningali sahihi, imara na mkunjufu,
Alhamdulillah, namshukuru Latifu.

Elimu nyingine waliyoipata ni ile tunayoiita elimu ya magharibi na alama ya kusoma katika enzi hizo ilikuwa ni Kiingereza. Mapacha hao wawili walikifahamu vilivyo



Sheikh Kaluta Amri Abedi



Sheikh Shaabani Robert

Kiingereza. Shaabani Robert alidhihirisha umahiri wake wa Kiingereza alipotafsiri shairi la Omar Khayam kutoka katika Kiingereza; '*Marudi mema*'.

Sheikh Kaluta Amri Abedi anadhihirisha uwezo wake wa kimombo anapoimba;

Ala za kuchuma sana, mimi pia nazijua
Kiingereza nakibana, fasihi wa kusifia
Nawashangaza mabwana, Wazungu na Waasia.

Ushahidi mwingine kuwa 'Kiingereza' nakibana ni pale Mwalimu Julius Kambarage Nyerere anapomshukuru kwa msaada wa kibingwa wa Sheikh Kaluta Amri Abedi akitafsiri kwa Kiswahili tamthilia ya William Shakespear; '*Julius Kaisari*'.

Hata hivyo Sheikh Kaluta Amri Abedi alikwenda hatua mbili zaidi ya Shaabani Robert katika kumudu lugha, kwani wakati Shaabani Robert alizimanya vilivyo lugha mbili Kiswahili na Kiingereza, Sheikh Kaluta Amri Abedi alifahamu Kiurdu, Kifarsy, Kiarabu na alikuwa amekwishaanza kujifunza Kifaransa.

Kwa upande wa kazi ya kuajiriwa wote kwa muda fulani walikuwa ni watumishi wakati wa Serikali ya kikoloni. Kwa miaka mingi Shaabani Robert alifanya kazi idara ya forodha na idara ya utunzani wa wanyama huko Mpwapwa. Yote yaliyompata huko ubaguzi wa rangi na uonevu amevieleza kwa ufasaha katika kitabu chake; '*Maisha yangu na baada ya miaka 50*'.

Sheikh Kaluta Amri Abedi kwa muda alifanya kazi idara ya posta na baadae alijiunga katika kazi ya kuhubiri dini ya Islam. Na hatimaye akaruhusiwa kuingia katika siasa na Hadhrat Khalifatul Masih II*ra* na kuwa Meya wa kwanza Mwafrika wa Dar es salaam, Mbunge wa Kigoma, Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Waziri wa Sheria na hatimaye Waziri wa Utamaduni na maendeleo ya jamii.

Inaonesha Shaabani Robert amejipambanua katika nyanja kadhaa za fasihi kwa mathalani riwaya, uandishi wa insha na alipozamia kabisa na kutengeneza jina ni kwenye ushairi. Hapa ni muhimu kukumbuka kwamba Shaabani Robert na Sheikh Kaluta Amri Abedi waliweza hata kutajana majina katika mashairi. Na hii ni dalili ya ukaribu waliyokuwa nao. Akimshukuru kwa kujiunga upande katika kile kitali cha 'Ndoa mbaya afadhali, kuliko ujana mwema' Shaabani Robert anamsifia Amri;

Heko Amri Abedi, mwenye fadhila na utu,
Heko ukidhi muradi, usitawi kati yetu,
Heko kijana asadi, katika biladi zetu,

Naye Sheikh Kaluta Amri Abedi akiwaeleza watesi kwamba hawana ubavu wa kupambana na Shaabani Robert anasema;

Kawashindeni mwawawazi, Shabani kwa tahakiki,
Na mpendao ulozi, na Shabani halogeki,

Sheikh Amri Abedi hakuwahi kuandika riwaya, lakini Shaabani Robert ana hazina za riwaya. Na falsafa inayotawala kazi zake za riwaya ni; '*Utu bora*', '*Ubinadamu*', '*Taadhima*', '*Sheria*' na '*Haki*'.

Sheria kwa Shaabani Robert ni msumeno wala sio chekecho lichagualo bila kujali haki na kweli. Mapenzi, dini, huwaunganisha binadamu kwa kuwaonea huruma masikini haya ndiyo aliyoyaamini na kusisitiza ya kwamba misaada tunayowapa siyo ihsani bali ni haki yao na matajiri ni wajibu wao kuwapa masikini.

Sheikh Kaluta Amri Abedi hakuwahi kuandika riwaya, isipokuwa aliwahi kuandika juu ya uhusiano wa mke na mme na maisha ya ndani. Kwa ujumla ameandika utangulizi katika baadhi ya diwani za Washairi. Ameandika utangulizi katika diwani ya Shaabani Robert; (*Kielezo cha Fasili*), Matiasi Mnyampala (*Waadhi wa ushairi*) na Akilimali (Snow white) (*Diwani ya Akilimali*).

Mapacha hawa wawili walitambua umuhimu na ulazima wa kuoa. Walielewa kuwa msingi wa ndoa ni '*Litaskunuu ilayhaa*' – ili kupata utulivu. (30:22).

Hata hivyo kama tutakavyoona, hawakupata utulivu saana ingawaje walijaaliwa kupata watoto. Shaabani Robert alioa mara mbili, kwani mke wake wa kwanza alifariki. Amina alikuwa libasi kwa Shaabani Robert na kumheshimu sana. Anasisitiza mwenyewe Shaabani Robert; Alikuwa johari ya maisha yangu, tegemeo na mshauri mwema. Kifo cha mke wake lilikuwa pigo kubwa kwake. Ni dhahiri kuwa kifo hicho kilileta hasara kubwa kwake binafsi hata hivyo katika uwanja wa fasihi tumepata moja ya shairi moja la huzuni na majonzi kuhusu mtu unayempenda. Na uhakika kuwa maisha hayatakwisha.

Endelea uk 11